# THE SACRED NAME BROADCASTER



## Mtangazaji wa Jina Takatifu

4/2025

a publication of **Assemblies of Yahweh**

THE SACRED NAME BROADCASTER

*An **Assemblies of Yahweh** publication.*
***Assemblies of Yahweh**, **The Narrow Way Newsletter**, **The Sacred Name Broadcaster**, **The Sacred Name Broadcast**, **The Sacred Scriptures**, **The Sacred Name Telecast**, and **WMLK Radio** are Service Marks and Trademarks of Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507*

***April 2025***
***Volume LVII, Number 1***

# YALIYOMO










***1 Jina la Yahweh katika Zaburi***

*Sifa zisizo na idadi za Mwenye-nguvu Yahweh zinaonyeshwa kote katika kitabu cha Zaburi. Zaburi hizi zinatufundisha na kutuhamasisha kama tunasoma na kuzitafiti kila siku.*

***13 Viumbe Vya Yahweh Vilivyoumbwa,sehemu ya 6***

*Mwenye-nguvu Yahweh aliumba madarasa manne ya viumbe kumtumikia Yeye. Basi tuhakikishe kwamba hatulegei kamwe katika kujitolea kwetu kama walivyofanya wengine.*


***18 Messiah katika Agano la Kale,sehemu ya 6***

*Fundisho la Agano Jipya la Messiah linathibitishwa kutoka kwa mafundisho ya Agano la Kale, ambayo yanaunda msingi wa Imani yetu.*

## Jalada Letu

*Daudi, mtunga –Zaburi mtamu wa Israeli, alionyesha upendo wake kwa Yahweh na kumwamini kwa moyo wote. Katika ujana wake, kama mchungaji wa mifugo ya babake, alijifunza jinsi ya kutunza na kulinda kondoo.*

*Daudi pia alikuwa mwanamuziki shupavukwenye vyombo vya nyuzi, kama vile kinubi. Jalada letu mwezi huu ni kiingilio kwa Mji wa Daudi katika Yerusalemu, ambacho kina kipengele cha kinubi.* ***"Kisha akajibu mmoja wa vijana akasema,Tazama nimemwona mwana mmoja wa Yese, Mbethlehemu, aliye stadi wa kupiga kinubi, tena ni mtu shujaa, hodari wa vita, anenaye kwa busara, mtu mzuri, ambaye Yahweh yu pamoja naye."*** *(1 Samueli 16:18).*




*Daudi alielezewa kama mtu baada ya moyo wake Yahweh mwenyewe, na, kwa sababu hii, alichaguliwa kuwa mkuu juu ya watu Wake. Daudi alionyesha upendo wake kwa Yahweh kwa zaidi ya Zaburi 72 zinazohusishwa naye. Kwa hivyo, tunaposoma kupitia kwa Zaburi, tunajawa na msukumo mkubwa na kuabudu kwa Yahweh- kutoka kwa kalamu ya kujieleza ya Daudi.*


*Wakati wowote tunahitaji msukumo, kutiwa moyo, na kuinuliwa kiroho, utayapata katika maandishi ya hekima ya Yahweh.* ***"Na wewe, Yahweh, U ngao yangu pande zote, utukufu wangu, anayeinua kichwa changu. Kwa sauti yangu nilimwita Yahweh, naye akaniitikia toka mlima wake mtakatifu. Selah."*** *(Zaburi 3:3-4).*

Mtangazaji wa Jina Takatifu huchapishwa kila mwezi na Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507. Uandikishaji wako umelipwa na watendakazi wenzi wenye hiari wa huduma hii ambao wanajali kwamba ujumbe huu wa wokovu unapaswa kutolewa bila malipo kwa ulimwengu wote kama shahidi kabla ya Ujio wa Pili wa Yahshua Masihi. Ingawa hakuna malipo yoyote yatakayotozwa kwenye chapisho hili, MICHANGO (yote inakatwa kodi) inakubaliwa kwa shukrani ili kusaidia kulipia gharama. Tunatumahi kuwa utashiriki katika kufanya habari hii ipatikane kwa wengine.

Nukuu zote katika The Sacred Name Broadcaster zimetolewa kwa The Sacred Scriptures, Bethel Edition, 1981, Assemblies of Yahweh, Bethel, PA 19507, isipokuwa ikitangazwa vingenevyo. Tafsiri zote za Biblia humu, zimesahihishwa ziwe thabiti na maandishi yaliyo ya awali zaidi yanayopatikana. Nakala za The Sacred Scriptures, Bethl Edition, zinapatikana. Kwa ujumbe jinsi ya kununua kopi yako, andika kwa Assemblies of Yahweh.

© Hakimiliki 2024 Assemblies of Yahweh. Haki zote zimehifadhiwa.
Malipo ya posta ya mara kwa mara huko Reading, PA 19612 (ISSN 879320). Simu (717) 933-4518. POSTA: Tuma fomu 3579 kwa Assemblies of Yahweh, SLP C, Bethel, PA 19507.

***Mwanzilishi na Mwandishi:** Mzee Jacob O. Meyer*



# Jina la YAHWEH katika Zaburi

*na Mzee Jacob O. Meyer*

Kuhakiki fundisho la Jina Takatifu ni muhimu, kwa sababu tunahubiri ujumbe huu kwa nguvu kubwa. Kwa sababu hiyo, ninaamini kwamba, katika Assemblies of Yahweh, lazima tuendelee kuhubiri mafundisho ambayo tunaamini na ambayo tunawasilisha kwa ulimwengu-mafundisho ambayo yako kwenye Biblia.

Zaburi zinayo sehemu ya kipekee sana katika historia ya Israeli. Hazikuhudumu tu kama muziki kwa ibada ya hekalu, lakini pia zilihudumu katika nafasi nyingine. Zilihudumu katika huduma ya Pasaka- ambayo ilikuwa maadhimisho ya kibinafsi ya Pasaka ya Yahweh, kwa sababu Yahshua na wanafunzi Wake katika chumba cha juu- ambayo haikuwa huduma ya hekalu- waliimba Sifa Kuu kabla ya kuenda nje usiku. Zaburi ni za kipekee katika historia ya Israeli, kwa sababu naweza kufikiria wakati wowote ninaposoma Zaburi, kwamba ninaweza kusikia kuimba ambako kulifanyika katika Hekalu la Yahweh, au pengine ninaweza kusikia watu wakitembea kupitia mitaa na kuimba nyimbo za moja ya Zaburi.

Daudi alikuwa na ushawishi muhimu sana juu ya Zaburi. Ikiwa ningekuuliza ni Zaburi ngapi zinabeba jina lake, ungeweza kuniambia? Karibu nusu ya Zaburi zinabeba jina la Daudi, kuthibitisha kwamba Daudi alikuwa na ushawishi wa kina juu ya Zaburi, kwani jina lake limeambatanishwa kwa 72 ya hizo. Ikiwa hilo linamaanisha kwamba

**Zaburi zinayo mahali muhimu katika maisha ya muumini. Ni vigumu kuwa na chochote katika Zaburi ambacho hakishughulikii hali ya aina ya kipekee ambayo inaweza kutokea katika maisha yetu.**

aliandika hizo zote, au baadhi yazo ziliandikwa kwa Daudi, kwa sababu maandishi ya juu katika Zaburi ni *leDavid,* ambayo inamaanisha ama *kwa,* au *na Daudi*. Hata hivyo, kutoka kwa hizo 72, kunaweza kuwa na zaidi ambazo zilikuwa uandishi wake. Kulikuwa na Zaburi ambazo ziliunganishwa, hivyo inaweza kuwa kwamba zaidi ya nusu yazo zilikuwa za uandishi wake. Daudi anaitwa mtunga-zaburi mtamu wa Israeli, na aliziunda kwa zaidi ya kipindi cha miaka 50, kutoka kwa wakati alikuwa akichunga kondoo, mpaka baadaye alipokuwa akitawala taifa la Israeli.

Zaburi zinayo mahali muhimu katika maisha ya muumini. Ni vigumu kuwa na chochote katika Zaburi ambacho hakishughulikii hali ya aina ya kipekee ambayo inaweza kutokea katika maisha yetu. Kama tunasoma kupitia Zaburi, tunaona kwamba maneno kuimba, kusifu, kubariki, na kutukuza Jina la Yahweh yanapatikana katika 32 ya Zaburi. Kwa mfano, kama utageuka kwa sura ya saba ya kitabu cha Zaburi, utapata hapo, ***"NitamshukuruYahweh kwa kadri ya haki yake."*** Katika Zaburi 7:17, ***"Nitaliimbia jina la Yahweh Aliye Juu."***

Katika 32 ya Zaburi, utapata maneno kama vile*: Liimbie Jina la Yahweh; lisifu Jina la Yahweh, libariki Jina la Yahweh;* na *litukuze jina la Yahweh***.**Moja ya mambo ambayo ninataka kuashiria kuhusu Zaburi ni kwamba ni mashairi ya Kiebrania. Hayana marudio ya sauti sawa, kama yanavyofanya mashairi ya Kiingereza, lakini yanao mwanguko na usambamba ambao ni wa kipekee katika ushairi wa Israeli. Ningependa kuashiria mambo kadhaa machache ambayo yatakusaidia kuelewa vizuri ushairi wa Kiebrania. Tunayo kozi katika Obadiah School of the Bible inayoitwa **Wisdom Literature** ambayo inashughulika na utafiti wa Zaburi na maandishi ya hekima ya Mithali, Mhubiri na Wimbo wa Suleimani.

Katika Zaburi ya tano, tutapata vipengele mbalimbali na mambo yanayohusiana kwa Jina la Yahweh. Ninatumai kwamba utakuwa umetiwa msukumo kama nilivyokuwa. Kila mara inanitia msukumo ninapotafiti hilo Jina na ubora na vipengele mbalimbali ambazo zinaambatanishwa kwa Jina la Yahweh. Kama tutaanza kwa mwanzo na kufanya kazi kupitia Zaburi, tukizingatia juu ya ambapo *jina* linatumika na mambo yanayotumika kwa Jina hilo- ukuu, utukufu wa Jina la Yahweh, tunaona kwamba Jina la Yahweh ni Jina kubwa. Moja ya mawazo yanayopenyeza zaidi yaliyonikujia, kama ninaangalia kwa Jina la Yahweh katika Zaburi, ni kwamba sifa ya kwanza ambayo inaambatanishwa kwalo, amri ya kwanza, ni upendo. Katika Zaburi 5:11, tunasoma hapo: ***"Nao wote wanaokukimbilia watafurahia; watapiga daima kelele za furaha, kwa kuwa Wewe unawahifadhi, walipendao jina lako watakufurahia. Kwa maana wewe utambariki mwenye haki; Yahweh utamzungushia radhi kama ngao."*** Hicho ni kifungu kikubwa!

Ni aina gani ya majina yanaambatanishwa kwa Jina la Yahweh? Ni nini uwanja wa ushirika? Uwanja wa ushirika ni kwamba wale ambao wanapenda Jina la Yahweh **watakuwa** wenye furaha. Wale ambao wanalipenda Jina la Yahweh watabariki Yahweh, na Yahweh atawabariki wale ambao wanaweka imani yao Kwake. Sasa, kama tunapenda kitu fulani, tutakilinda, sivyo? Hili ni wazo muhimu sana ambalo linaendana na neno *upendo*. Yahweh anatupenda sisi, na anatulinda sisi. Tunalipenda jina la Yahweh sana hivyo kwamba tutalilinda Jina hilo? Sasa, linganisha katika mstari wa 10 nini Yahweh anajaribu kutuambia sisi katika Zaburi hii iliyoongozwa, ambayo ni Zaburi ya Daudi. ***"Wewe, Elohim, uwapatilize, na waanguke kwa mashauri yao. Uwatoe nje kwa ajili ya wingi wa makosa yao, kwa maana wamekuasi wewe."*** Tunalipenda Jina la Yahweh sana hivyo kwamba hatutakuwa sehemu ya uasi? Hiyo ndiyo Zaburi ya tano inahusu yote. Kama utaangalia kwa maisha ya Daudi, unaweza kuona kwamba alikuwa amezungukwa sana karibu kwa kila wakati wa maisha yake. Alikuwa na maisha magumu, kwamba ilionekana kuathiri yeye, vile vile baadaye maishani.

Katika Zaburi 5, matumizi ya neno *upendo* lililoambatanishwa kwa Jina- sifa ya kwanza ni kwamba tutapenda, kulinda, kuheshimu, kubariki, na tutakuwa na furaha- kwa sababu Yahweh ametupa Jina Lake. Huu ni Ukweli mkubwa. Kwa hivyo, inapaswa

kutufanya wenye furaha. Sasa, kumbuka, ni nini Mtume Paulo anasema ni matunda ya Roho Mtakatifu? Ya kwanza ni upendo- ya pili ni furaha. Ninashangaa ni wapi aliyapata? Ikiwa unafikiria aliyapata kutoka kwa Zaburi 5, ningekubaliana.

Katika Zaburi 8:1: ***"Ee Yahweh, Elohim wetu jinsi lilivyo tukufu jina lako duniani mwote…."*** Unaamini kwamba jina la Yahweh ni Jina bora? Neno la Kiebrania hapa ni *'addir*, na ni kutoka kwa #142 katika **Strong's Concordance***, kupanua, kuwa kuu au tukufu*, Ee Yahweh, Elohim wetu, Mfalme wetu, jinsi bora, jinsi lilivyo tukufu, jinsi lilivyo kuu Jina Lako katika dunia yote. Ni nini tunafanya kutukuza Jina la Yahweh? Tunafanya nini kulifanya Jina hilo kuu na tukufu? Tunatimiza mwito wetu? Tunafanya kila kitu katika nguvu yetu kulifanya Jina hilo kubwa, ili kwamba watu wote wa dunia hii watalijua?

Gundua pia mstari wa 9, ambao ni sawa kabisa kama mstari wa 1. Anasisitiza mawazo kwamba anaonyesha hapa kama anaangalia nini imemzunguka kando yake, na analinganisha binadamu kwa fahari ya uumbaji wa Yahweh anasema, "Mtu ni kitu gani?" Si chochote.Na bado Yahweh ameweka chini ya miguu yake vitu vyote. Sasa hili linafanya Jina la Yahweh kuwa tukufu. Unafikiria kaka na dada kwamba tunapaswa kuwaheshimu wale ambao wako juu yetu? Hili ndilo mtunzi wa Zaburi anajaribu kutuambia sisi. Mheshimu Yahweh, kwa sababu yuko juu yetu. Lifanye Jina la Yahweh kuu. litukuze (*'addir* katika Kiebrania), na kulifanya tukufu. Lichapishe ili kwamba watu wataweza kuliheshimu.

Katika Zaburi 9:9-10, bado tunapata kipengele kingine na ubora. ***"Yahweh atakuwa ngome kwake aliyeonewa, Naam, ngome kwa nyakati za shida. Nao wakujuao jina lako wakutumaini wewe; maana wewe Yahweh hukuwaacha wakutafutao."*** Tambua neno kujua hapa. Kujua Jina inamaanisha nini? Inamaanisha wokovu. Wokovu- ni kimbilio. Mithali 18:10 inasema, ***"Jina la Yahweh ni ngome imara; mwenye haki huikimbilia, akawa salama."*** Katika Zaburi 91:14b: "***Nitamweka palipo juu, kwa kuwa amelijua jina langu."***

Dr. Leon Wood, katika kitabu chake **A Survey of Israel's History**, alifanya taarifa kwamba Kutoka 6:3 haipaswi kutafsiriwa kwani wazee hawakutumia Jina la Yahweh. Nimekuwa nikisisitiza hili ni kweli kwa muda mrefu sana, hapa ni msomi ambaye anaunga mkono yale niliyoyasema. Wazee hawakuelewa maana ya kweli ya Jina la Yahweh. Tambua hapa, kwamba Yahweh atakuwa kimbilio kwa walioonewa, kimbilio katika Dhiki Kuu. Hilo ndilo Kiebrania inasema wakati mkuu wa shida. Hilo linatumika kwetu.Kuwa tayari kujua Jina la Yahweh. Tunajua na kuelewa umuhimu wake- maana ya ndani, muhimu iliyopo hapo? Hii ni nini nimekuwa nikijaribu kuonyesha kwa watu wa duinia hii, kwamba ni zaidi kuliko tu kusema Jina hilo. Ni kujua linamaanisha nini. Ni kujua Aliye na Nguvu ambaye anasimama nyuma ya Jina hilo- kujua nini aliye na kwa nini anafanya mambo kama anavyoyafanya. Hivyo unaweza kuona, kama tunalijua Jina la Yahweh, tutaweka imani yetu katika Yeye, kwa sababu hakuna Jina lingine ambalo litatupea wokovu. Hakuna Jina lingine ambalo lina maisha ya milele yameambatanishwa kwake.Kujua Jina la Yahweh inamaanisha kupata ulinzi- kimbilio katika nyakati za shida- katika dhiki kuu.Kwa nini tuko hapa? Si sababu tunahisi, kama Nuhu alivyofanya, kwamba hukumu iko tu mbele?

Katika historia ya ulimwengu, hakujawahi kuwa na wakati ambapo kumekuwa na uharibifu mwingi hivyo. Uharibifu huu umeweza kuonyeshwa kama kuwa kawaida. Sio kawaida kwa watu kutenda kama wanavyotenda kwa miaka 10 hadi 20 iliyopita. Ni kwetu sisi kutambua kwamba hukumu ya Yahweh iko tu mbele yetu. Ikiwa tunataka ulinzi wakati wa dhiki, lazima tujue Jina hilo pekee na kwamba jina hilo pekee litaweza kutoa kwetu maisha ya milele. Walakini, lazima tuwe watu wenye haki kama tutaweza kutumia Jina hilo.

Tambua katika Zaburi 20 kwamba Jina la Yahweh linatetea. Zaburi 20:1: ***"Yaweh akujibu siku ya dhiki*** [tena, pengine rejelo kwa Dhiki ile]; ***Jina la Elohim wa Yakobo likuinue juu…."*** Hiyo inamaanisha lazima tuamini katika Jina. Neno *kutetea* katika Kiebrania linamaanisha kuwa na uadilifu, na litakuwa linatetea, au kulinda, wale ambao wanajua Jina la Elohim wa Yakobo- Jina la Yahweh. Tambua usambamba wazi hapa. Neno *Jina la Elohim wa Yakobo* ni sambamba kwa Yahweh katika mstari wa kwanza, na *kusikia katika siku ya shida* ni sambamba kwa kulinda. Yahweh atasikia, na haimaanishi kwamba atakuwa tu anasikiliza na hafanyi kitu, lakini atalinda. Atawalinda wale ambao wana uadilifu. Ni wazo bora sana.

Mstari wa 5: ***"Na tuushangilie wokovu wako, kwa jina la Elohim wetu tuzitweke bendera zetu: Yahweh akutimizie matakwa yako yote."*** Hili linaongea kuhusu nini? Kuinua bendera inamaanisha- kama tu katika Biblia na kama tu leo- kukusanya watu wa Yahweh, kuunganisha

vikosi vyetu, kuvileta pamoja katika umoja, katika moja. Neno *beramu* hapa katika Kiebrania, *dagal* ni neno sawa ambalo lilipaswa kutafsiriwa beramu katika Ufunuo 19. ***"Na tuushangilie wokovu wako, kwa jina la Elohim wetu tuzitweke bendera zetu."*** Hilo ndilo linapaswa kuwavuta watu wa Yahweh pamoja- Jina la Yahweh. Endelea na mistari iliyobaki ya 5-7: ***"Yahweh akutimizie matakwa yako yote. Sasa najua kuwa Yahweh amwokoa aliyetiwa mafuta wake; atamjibu toka mbingu zake takatifu, kwa matendo makuu ya wokovu ya mkono wake wa kuume. Baadhi wanatumainia magari na hawa farasi, bali sisi tutalitaja jina la Yahweh Elohim wetu."*** Hivyo Jina la Yahweh ndilo litatulinda sisi. Nini ilimlinda Gideoni, nini ilimlinda Baraki, na nini ilimlinda Daudi katika vita vyake na Goliathi? Halikuwa Jina la Yahweh?Daudi anasema, *"Naja kwako katika Jina la Yahweh, Elohim wetu. Unakuja kwangu na upanga na fimbo. Lakini naja kwako katika jina la Yahweh, Elohim wetu."* Jina la Yahweh litatulinda, na litakusanya watu wa Yahweh pamoja. Kama tu, Israeli alivyokuwa chini ya nguzo ya wingu na moto walipotoka Misri, ulinzi huo ulikuwapo dhidi ya Farao na jeshi lake. Lakini hatuwezi kupata ulinzi isipokuwa tuwe tumeungana chini ya beramu ya Yahweh.

Katika Zaburi 22:22: ***"Nitalitangaza jina lako kwa ndugu zangu, katikati ya kusanyiko nitakusifu."*** Zaburi 22 ni rekodi ya nini ilifanyika wakati Yahshua aliye Messiah alitundikwa. Ni unabii wa kutundikwa kwa Yahshua. Fahali, Efraimu, katika mstari wa 12- fahali wenye nguvu wa Bashani- inahusiana kwa kabila 10 za Israeli ambao walimkataa wakati huo. Pia, simba wa kabila la Yuda katika mstari wa 13 inahusiana kwa Wayahudi na Wabenyamini ambao walimkataa Yahshua na kuuzunguka mti wake alipouawa.

Anasema katika mstari wa 22 kwamba ***"Nitalitangaza jina lako...."*** Daima nilifikiria kwamba hapa palikuwa mahali pa pekee ambapo palijadili tamko la Jina la Yahweh. Katika Zaburi 102, utapata karibu kitu sawa. Katika Zaburi 102:21: ***"Watu walitangaze jina la Yahweh Sayuni, na sifa zake katika Yerusalemu...."*** Tuna wajibu kulitangaza na kuhubiri Jina la Yahweh, na wale ambao ni watu wa Yahweh watakuwa wanafanya hili, kama tu alivyofanya Yahshua. Hakurudi nyuma. Kama nilivyoandika katika karatasi mingi ambazo nilitayarisha kwa madarasa mbalimbali, watu waliangalia kwa karatasi hizo za muhula, na wamesema, "Huogopi kukabidhi karatasi kwa profesa ukitumia Jina la Yahweh na ukitumia Jina la Yahshua?" Nilisema, "Hapana, wanajua kuwa ni Ukweli. Kwa nini? Kwa nini nisilitangaze?" Yahshua hakurudi nyuma kwa sababu Mafarisayo walisema usilitumie Jina. Yahshua alilitangaza, na watu wa Yahweh watalitangaza- wale ambao ni waaminifu kwa Neno Lake.

Zaburi 29 ni Zaburi ambayo inatia hofu kwa wale ambao wanaisoma. Awali niliitafsiri Zaburi 29 moja kwa moja kutoka kwa Kiebrania, na hata inatia moyo zaidi katika lugha ya Kiebrania kuliko ilivyo katika Kiingereza. Nguvu na hofu ambazo zinatokana na Jina la Yahweh zinakuja wazi kabisa katika kifungu hicho. ***"Mpeni Yahweh, enyi wana wa El.*** [Elim, au wenye nguvu. Kiandiko katika **Companion Bible** kinasema malaika, au pengine, tungeweza kusema wajumbe]. ***Mpeni Yahweh utukufu na nguvu Mpeni Yahweh utukufu wa jina lake; mwabuduni Yahweh kwa uzuri wa utakatifu*** [au katika patakatifu pazuri]." Kisha anaendelea kuelezea Jina la Yahweh, na yale sauti ya Yahweh inafanya. Ngurumo saba zimerekodiwa katika Zaburi 29. Inakuambia katika Ufunuo 10, usiandike yale ngurumo saba zinasema, yatie muhuri. Ngurumo saba zinahusiana kwa mamlaka ya Yahweh katika uumbaji Wake. Katika Zaburi 29, inajitokeza wazi sana kwamba kunazo ngurumo saba. ***"Sauti ya Yahweh i juu ya maji: El wa utukufu alipiga radi...."*** Sauti yake inahusiana kwa ngurumo Zake- yale anayosema. ***"Aivunja-vunja mierezi ya Lebanoni. Airusha-rusha kama ndama. Sauti ya Yahweh yaipasua miali ya moto.Sauti ya Yahweh yalitetemesha jangwa, Yahweh alitetemesha jangwa la Kadeshi. Sauti ya Yahweh yawazalisha ayala, na kuifichua misitu na ndani ya hekalu lake wanasema wote, utukufu."*** Katika toleo **la King James,** nitafsiri mbaya kwa sababu Kiebrania inasema, *"Na katika hekelu lake kila kitu kinasema, utukufu."* Hivyo kunao utukufu unaotokana kwa Jina la Yahweh, na ni utukufu ambao unahusiana kwa nguvu Yake inayoonyeshwa katika sauti ya ngurumo.

Katika Zaburi 33, tunapata kipengele kingine cha nini Jina la Yahweh linamaanisha katika kitabu cha Zaburi, ubora ambao umeambatanishwa kwa Jina la Yahweh katika Zaburi 33:18. ***"Tazama, jicho la Yahweh li kwao wamchao, wazingojeao fadhili zake. Yeye huwaponya nafsi zao na mauti, na kuwahuisha wakati wa njaa. Nafsi zetu zinamngojea Yahweh; yeye ndiye msaada wetu na ngao yetu. Maana mioyo yetu itamfurahia, kwa kuwa tumeli-***




***tumainia jina lake takatifu."*** Kunao ulinzi tena, kama tulivyoona awali. Kama utarudi nyuma kwa Zaburi 3:3, inatuambia kwamba Jina la Yahweh ni ngao. ***"Na wewe, Yahweh, U ngao yangu pande zote, utukufu wangu na mwinua kichwa changu."*** Ngao hapa inahusiana kwa ulinzi, na Yahweh ataweza kutupa ulinzi. Fikiria kuhusu hilo na ulihusishe kwa Goliathi wa Gathi. Goliath alikuwa na mtu Fulani aliyeenda mbele yake akiwa na ngao kumlinda kwa shambulio la Daudi. Lakini Daudi alikuwa na nini? Alikuwa na kitu fulani chenye ulinzi zaidi; kwa sababu kilikuwa Jina la Yahweh. Jina la Yahweh lilimzunguka kama tu vyombo vya kivita. Hakuna yeyote ambaye Yahweh ameweka Jina Lake juu yake anapaswa kuwa na wasiwasi wowote kuhusu ulinzi.

Katika Zaburi 34:1: ***"Nitambariki Yahweh kila wakati: sifa zake zi kinywani mwangu daima.Katika Yahweh nafsi yangu itajisifu, wanyenyekevu wasikie wakafurahi. Mtukuzeni Yahweh pamoja nami, na tulikuze jina lake pamoja."*** Neno *kutukuza* katika Kiebrania ni *gadal*, na linamaanisha *kufanya kubwa, kuheshimu*. Ifuatayo tutazingatia neno *kuinua*. Basi na tuinue Jina Lake. Neno kuinua katika Kiebrania ni *rum*, na linamaanisha *kuinua*. Kwa nini tuliinue Jina la Yahweh? Kwa sababu limekuwa likikanyangwa chini ya watu wa kidini kwa muda mrefu. Jina Yahweh limekanyangiliwa chini na usomi. Limekanyangiliwa chini na jamii ya kidini ya Kiyahudi. Basi tutoe heshima kwa Yahweh. Basi tulikuze, na kulifanya kuu – *gadal*- na basi tuliinue kwa nafasi ya juu yetu kama beramu. Tunapoinua kitu juu, inamaanisha kwamba tunakiinua kwa heshima yetu. Neno *rum* hapa lina maana ya kuinua Jina la Yahweh katika heshima ya watu.

Tambua pia, kwamba ili kuifanya, lazima tuifanye pamoja. Mara kwa mara kote katika Zaburi, nimeona umoja, umoja wa watu wa Yahweh, umoja ambao tunao katika Yahshua aliye Messiah- umoja ambao tunao katika Jina lake. Tambua hilo tena: ***"Mtukuzeni** [gadal] **Yahweh pamoja nami, na tulikuze** [rum] **jina lake pamoja."*** Basi tuinue Jina Lake pamoja. Hatuwezi kulifanya kwa sisi wenyewe. Hatuwezi kuifanya kibinafsi, lakini lazima tuifanye kama kitengo, kama kikundi. Kisha tutaheshimiwa katika jamii ya nje. Watu wataona kwamba sio tu mtu mmoja, lakini kwamba ni sisi sote tunalifanya pamoja.

Katika Zaburi 44, tunapata kipengele kingine cha Jina la Yahweh. Katika Zaburi 44:4: ***"Ee Elohim, wewe ndiwe mfalme wangu, uagize mambo ya wokovu kwa Yakobo. Kwa nguvu zako tutawaangusha watesi wetu; kwa jina lako tutawakanyanga watupingao."*** Fikiria kuhusu hili kwa dakika chache na kuihusisha kwa nyakati za mwisho wakati Dhiki Kuu inaposhambulia, na watu wa Yahweh wanakabiliwa kwa mateso makubwa. Kifungu hiki ni cha kinabii kwa wakati huo wa Dhiki, kwa sababu, katika Malaki 4:3, inasema, ***"Nanyi mtawakanyanga waovu; maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu katika siku ile niifanyayo, asema Yahweh wa majeshi."*** Hapa tunapata, kupitia Jina la Yahweh tutawakanyanga chini ambao watainuka dhidi yetu, na, kisha, mstari wa 6: ***"Maana sitautumainia upinde wangu, wala upanga wangu hautaniokoa. Bali wewe ndiwe uliyetuokoa na watesi wetu; na watuchukiao umewaaibisha."*** Hili ndilo hasa nini itafanyika wakati Ufalme wa Yahweh unaanzishwa duniani humu.Yahweh ataweza kuteteta watu Wake. Watainuliwa juu, na watu wa jamii ya kidunia watashushwa chini.

Kunacho bado kifungu kingine katika Zaburi 44 ambacho tunahitaji kukumbuka.Kinapatikana katika moja ya nyimbo katika kitabu cha wimbo chetu.***"Hata utuponde katika mahali pa mbwa-mwitu, na kutufunika kwa uvuli wa mauti."*** (Zaburi 44:19). Shetani hajawasonga watu wa Yahweh? Wakati wowote Yahweh anataka kujaribu mtu fulani, anamwachilia Shetani juu yake, kama tu alivyofanya na Ayubu. Anaondoa ulinzi Wake kwa muda, na Shetani anashambulia juu ya huyo mtu binafsi, akijaribu kumwangamiza. Joka inawakilisha Shetani katika Ufunuo 12:9. Ingawa umetuvunja na kutuumiza katika mahali pa Shetani [ninaingiza ndani utafsiri] na kutufunika kwa kivuli cha mauti [kama tu Ayubu]. Ayubu lazima alikuwa katika hali ya kutisha wakati marafiki zake hawangeongea na yeye kwa wiki kwa woga kwamba angekufa ikiwa wangesema kitu fulani. Walifikiria kwamba angeweza kuaga kama hata wangejiwasilisha wenyewe hapo kwake, kwamba kama angejigeuza mwenyewe kando, ingeweza kuwa uharibifu wake. Waliketi hapo wiki nzima na hawakuongea, kwa sababu alionekana mbaya sana.

***"Ikiwa tumelisahau jina la Elohim wetu, au kumnyoshea el mgeni mikono yetu; je! Elohim hatalichunguza neno hilo? Maana ndiye azijuaye siri za moyo."*** (Zaburi 44:20-21). Vipi tumefanya hili? Watu wa Yahweh lazima wajifunze kuchoma daraja nyuma yao. Lazima tujifunze tusisikilize kwa watumishi hao ambao wanahubiri katika majina ya upagani na kuhubiri uwongo. Kama tutauruhusu uabudu katika majina ya upagani kuingilia kati kwenye ibada ya Yahweh, itazuia na kuzima Roho Mtakatifu wa Yahweh.

"***Ikiwa tumelisahau jina la Elohim wetu, au kumnyoshea El mgeni mikono yetu***,[kumaanisha katika uabudu kwa el wa kigeni], bila shaka Yahweh ataichunguza, kwa sababu anajua siri za mioyo yetu. Hatuwezi kuficha chochote kwake, kwa sababu anaweza kuangalia ndani kabisa kwenye mioyo yetu na kuona nini iko hapo. Nini inafanyika tunapoanza kusahau Jina la Yahweh? Yahweh ataweza kutukataa. Nini inafanyika kama tunaanza kunyoosha mikono yetu kwa el wa kigeni- kuabudu katika jina la uwongo, au katika mafundisho ya uwongo? Yahweh atatufagia tu kando. Ilimbidi aifanye kihalisi na mamilioni ya watu katika nyakati za kibiblia. Fikiria kuhusu hilo kwa dakika: Kunaye yeyote wa watu ambao Yahweh alileta kutoka Misri aliyeenda kwenye Nchi ya Ahadi? Ni wawili tu wao, Kalebu na Yahshua, walikuwa waaminifu. Wengine wote (zaidi ya watu milioni 2) walikufa nyikani, kwa sababu hawakuwa waaminifu kwa Yahweh. Yahweh hataweza kuleta kwenye familia Yake, mtu yeyote ambaye si mwaminifu, yeyote ambaye ananyoosha mikono yake kwa el wa kigeni.

Hiyo ni moja ya sababu kwa nini tumechapisha **The Sacred Scripture,** *Bethel Edition*. Kwa miaka, ilitubidi kuweka akili zetu kuondoa M-ngu na Bw-na tulipokuwa tunasoma na kusoma Yahweh na Elohim badala yake. Sasa tunayo Biblia bora ambayo imerekebisha kumi ya maelfu ya makosa ya utafsiri ambayo yanapatikana katika toleo la **King James** na toleo zingine vile vile. Kiasi kipi cha majina ya upagani bado kinaambatana nasi? Tumeweza kuondoa majina ya Maabali kutoka kwa midomo yetu, Hosea 2:16?

Zaburi 48:9 ***"Tumezitafakari fadhili za upendo zako, ee Elohim, katikati ya hekalu lako. Kama lilivyo jina lako, Ee Elohim, ndivyo na sifa yako hata miisho ya dunia: mkono wako wa kuume umejaa haki."*** Tunapoona hili *fadhili za upendo* katika Kiebrania lina maana ya-*huruma*, na linakuja kutoka kwa neno la Kiebrania *chesed*. Linamaanisha kwamba Yahweh anayo huruma, na kwamba Yahweh anasamehe wale ambao wanaweza kukosea amri Zake wakati hawafanyi hivyo kwa makusudi.

Kisha anasema ***"Kama lilivyo jina lako, Ee Elohim, ndivyo na sifa yako hata miisho ya dunia: mkono wako wa kuume umejaa haki."*** Unapohusisha hilo nyuma kwa mwanzo wa mstari wa 9, tunaweza kutarajia fadhili za upendo na huruma, kulingana kwa Jina la Yahweh. Hilo linamaanisha nini? Jina la Yahweh linamaanisha milele, wa milele. Wakati watu wa Yahweh ni wenye dhati na waaminifu, wanaweza kutarajia huruma na *chesed* milele, kwa sababu Yahweh ni mwenye haki. Yeye sio asiye na msimamo. Habadili akili Yake kutoka siku hadi nyingine. Hatabadilika nyuma na kusema, *"Basi, nilikusamehe mara moja, lakini leo sitakusamehe."* Yoyote aliyoahidi ndilo atatimiza. Huo ni ukuu wa Jina la Yahweh, kwa sababu anao umilele kufanya kazi, sio tu miaka michache, kama afanyavyo binadamu.

Katika Zaburi 52:8: ***"Bali mimi nikama mzeituni umeao katika nyumba ya Elohim*** [kumbuka, mti huu mzeituni wa kijani katika nyumba ya Yahweh unahusiana kwa mashahidi wawili]: ***Nitazitumai fadhili za Elohim milele na milele*** [milele na milele inahusiana tena kwa Jina la Yahweh]. ***Nitakushukuru milele kwa maana umetenda; nitalingojea jina lako kwa kuwa ni jema, mbele ya watakatifu wako"*** Kutumaini kwa Jina inamaanisha kwamba tutaweza kuwa tu kama



***"Bali mimi ni kama mzeituni wa kijani umeao katika nyumba ya Elohim. Nitazitumai fadhili za Elohim milele na milele Nitakushukuru milele kwa maana umetenda; nitalingojea jina lako kwa kuwa ni jema, mbele ya watakatifu wako."***

ZABURI 52:8

Musa- mti wa mizeituni wa kijani katika Nyumba ya Yahweh. Musa hakuathirika vyovyote kwa miaka 120 ya uwepo alioishi. Maisha yake yaliendelea, na alikuwa mti safi, wa kijani unaozaa hadi kwa wakati wa kifo chake.

Watu wanakufa vifo vya kutisha hivyo leo. Ninafikiria mwenyewe, kweli, Yahweh hajaanza kuwahukumu kwa kufungua magonjwa hayo yote yenye uchungu juu ya watu wa ulimwengu huu? Baadhi ya watu wanasema, "Eee, ni Mwenye-nguvu. Tunamlaumu Yeye. Hakuwezi kuwa na Mwenye-nguvu anayeruhusu watu wateseke namna hiyo!" Kisha wanamshtaki na kumpa changamoto Yahweh: "Kwa nini hakuwezi kuwa na Mwenye-nguvu, kwa sababu anawaruhusu watoto wachanga wafe!" Na bado, unaona, vifo hivi ni matokeo ya dhambi, na watu hawaelewi kwamba dhambi inabeba adhabu. Adhabu-mshahara wa dhambi- ni kifo. Basi tusimpe changamoto Yahweh. Basi tusimshtaki kwa uongo. Basi tuweke lawama ambapo inastahili na kwamba hiyo ni juu ya binadamu na asili yake ya kimwili, na dhambi (uasi wa Sheria) anayoifanya. Ninakaa nikitafakari wazo hilo: Ni nini Yahweh anastahili kufanya kuwasababisha watu hawa kufikiria? Kwa nini wasianze kufikiria: lazima tunafanya kitu fulani kimakosa. Kwa nini wasianze kujichunguza wenyewe katika mwanga wa Maandiko badala ya kumpa changamoto Yahweh? Kisha wangekuwa kama mti wa mzeituni wa kijani katika Maandiko.

Watu wa kale muda wao uliisha tu. Hakukuwa na uchungu huu wote kabisa, uvimbe wa saratani na magonjwa ambayo yanaendana na kifo leo. Walifikia umri fulani, na wakaaga tu. Hakukuwa na uchungu unaochelewa, kifo cha kutisha kinachoumiza, kupewa madawa kama ilivyo leo. Hivyo basi tuwe waaminifu kwa Yahweh ili kwamba tutaweza pia kuhifadhiwa kwa aina hiyo ya kifo cha uchungu.

Katika Zaburi 54:1: ***"Ee Elohim, kwa jina lako uniokoe…."*** [Unaona, niokoe mimi kwa Jina Lako.] ***"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina lingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa."*** (Matendo ya Mitume 4:12). ***"Ee Elohim, kwa jina lako uniokoe, na kwa uweza wako unifanyie hukumu. Ee Elohim, uyasikie maombi yangu, uyasikie maneno ya kinywa changu."*** (Zaburi 54:1-2). Kuokolewa kwa Jina. Fikiria kuhusu hilo- hii kweli ni imani ya miujiza tuliyonayo. Assemblies of Yahweh ni dini ya miujiza, na sisi ni miujiza- miujiza inayotembea, kwa sababu Yahweh, kwa nyakati mingi katika wakati uliopita, aliwaokoa wengi wetu kutoka kwa uharibifu fulani, Zaburi 103:1-6.

Zaburi 61:5: ***"Maana wewe, Elohim umesikia nadhiri zangu. Umewapa urithi wao waliogopao jina lako.Utaziongezea siku za mfalme; miaka yake itakuwa kama vizazi vingi. Atakaa mbele za Elohim milele: ziagize fadhili na kweli***

***zimhifadhi. Ndivyo nitakavyoliimbia sifa jina lako daima, ili niondoe nadhiri zangu kila siku."*** Tunaamini hilo? Tunaamini kwamba Yahweh amesikia ahadi ambazo tumefanya kwake? Ningependa kuhusisha hili kwa ushauri wa ubatizo.Tunapoenda katika ushauri wa ubatizo, kila wakati naambia watu kwamba wanaapa kiapo kwa Yahweh, na anasikia kiapo hicho. Itarekodiwa na kuandikwa chini na malaika kwa sababu hilo ndilo tunasoma katika Mhubiri 5:4-7.

Katika mstari wa 5: ***"Maana wewe, Elohim umesikia nadhiri zangu. Umewapa urithi wao waliogopao jina lako...."*** Sasa ruhusu tufikirie kuhusu neno urithi. Neno urithi (*heritage*) linamaanisha (*inheritance*) *urithi*. Urithi upi Yahweh ameahidi kwa wale ambao wanaogopa Jina Lake? Kwanza kabisa, wokovu- kuokolewa kwa milele yote, kwa sababu Jina la Yahweh linamaanisha milele, uwepo wa milele. Pili Danieli 7 inaahidi kwamba Watakatifu wa Aliye Juu watauchukua Ufalme wa Yahweh. Umejitayarisha kwa hilo?

Watu wengi wanasema, "Ee, nitatawala katika ufalme, na wanasisitiza kwamba watakuwa wanatawala katika ufalme." Ninashangaa kama wanaweza hata kujitawala wenyewe sasa hivi? Yahweh anatupima sisi, anatuelimisha, na kutujaribu sisi. Ndugu hatuwezi kuanguka yoyote ya mitihani hii. Kama tutamwangusha Yahweh, hatutapokea hifadhi katika mnara wenye nguvu huo, kama inavyosema katika Zaburi 61:3. ***"Kwa maana ulikuwa kimbilio langu, ngome yenye nguvu adui asinipate. Nitakaa katika hema yako milele: nitaikimbilia sitara ya mbawa zako."*** Watu wanasema: "Nitakuwa nyumbani na Yahweh." Ataweza kutukubali sisi kwenye nyumba Yake?

Mambo hayo yote kaka na dada, tutaweza kufikiria kuyahusu. Hatuwezi tu kusema: "Nitaweza kutawala," kwa sababu Yahweh ataweza kufanya uteuzi wa ambaye atatawala na Yahshua katika Ufalme. Kunayo mengi ambayo lazima tutimize kabla ya mwishowe kupata aina hiyo ya utume.

***"Nitakaa katika hema yako milele, nitaikimbilia sitara ya mbawa zako. Selah. Maana wewe, Elohim umezisikia nadhiri zangu: umenipa urithi wao waliogopao jina lako."*** (Zaburi 61:4-6). Mimi ni mwaminifu kwa viapo hivyo. Wewe je? Hii ndiyo hoja ambayo Daudi anafanya katika Zaburi 68, ambayo ni Zaburi ya kutia msukumo sana kwangu. Ninaizingatia kuwa Zaburi ya Vibanda kwa sababu kadhaa. Inaelezea wataalamu, wakipanda kwa Vibanda, na hekalu ya Yahweh katika Yerusalemu. Pia ni Zaburi, au [*mizmor shir (mizmor*), zaburi au wimbo wa Daudi]. Zaburi 68:4: ***"Mwimbieni Elohim, lisifuni jina lake, Mtengenezeeni njia ya barabara, apiitaye majangwani kama mpanda farasi; Jina lake ni Yah...."*** Watafsiri hawangeweza kuondoa kila tukio la Jina Takatifu kutoka kwa Biblia, wakijaribu jinsi wangeweza. Katika mstari huu, ilibidi kuiacha, kwa sababu Jina Lake ni Yahweh, sio Bw-na. Tunayo nakala ya toleo la **Geneva Bible,**na angalia na tazama, tunagundua kwamba Jina liliwachwa katika **Geneva Bible** kama Yah miaka 100 kabla ya toleo la **King James** kutafsiriwa. Kama unaweza kuliangalia wakati fulani, utapata hilo kuwa la kuangazia. Ni la kutia msukumo kweli kwangu, kwa sababu watafsiri walikutana na hili katika **Geneva Bible** na wakasema, "Basi lazima ni la umuhimu au watafsiri wa **Geneva Bible** hawangeliacha hapo. Hivyo basi, nasi pia tuliache hapo." Katika Zaburi 68:4, katika **King James**, tunaambiwa kumsifu Yeye, na neno *kusifu* linamaanisha *kusifu*, au *kubariki* Yahweh kwa Jina lake Yah.

Katika Zaburi 69:35, tunapata: ***"Maana Elohim ataiokoa Sayuni, na kuijenga miji ya Yuda, na watu watakaa ndani yake na kuimiliki. Wazao wa watumishi wake watairithi, nao walipendao jina lake watakaa humo."*** Karibu tu katikati mwa Zaburi tunapata rejeleo lingine kwa kupenda Jina na ahadi kwa kukaa hapo ndani- ya kuwa katika urithi huo.

Katika Zaburi 72, kuanzia mstari wa 17, tunayo Baraka kwa nusu ya kwanza ya Zaburi. Kitabu cha Zaburi kinaweza kuwekwa kwenye sehemu tano zinazohusiana kwa vitabu vya kwanza vitano vya Torati. Kitabu cha Walawi kinaanzia na Zaburi 73. Vitabu vya Hesabu na Kumbukumbu la Torati vinafuata hili, kama nilivyofunza kwa wale ambao wamechukua kozi ya utafiti wa Zaburi ambayo nimefundisha katika Obadiah School of the Bible. Zaburi 72:17: ***"Jina lake na litadumu milele...."*** Sasa, ikiwa litadumu milele, kwa nini watu hawalitumii leo? Tena ninataka kuashiria kwamba neno Jina ni la umoja.

Neno *kudumu* lina maana ya *kudumu, kubaki milele- olam* katika Kiebrania- wakati nje ya akili.***"Jina lake na lidumu milele kama jua*** [kwa nini hawalitumii leo? Bado jua liko hapo]; ***Na watu watabarikiwa kwake, mataifa yote na wamwite heri. Na ahimidiwe Yahweh, Elohim, Elohim wa Israeli, Atendaye,miujiza yeye peke yake. Jina lake tukufu na lihimidiwe melele, dunia yote na ijae utukufu wake."*** Unaweza kuona hapa kwamba



***"Mara ngapi nimetaka kuwakusanya watoto wako kama vile kuku avikusanyavyo vifaranga vyake chini ya mbawa zake...."***

LUKE 13:34B

kunayo baraka, lakini pia maombi. Mzaburi Daudi anawaambi watu kukumbuka- kuheshimu- Jina la Yahweh. Jina lake litadumu milele ilmradi jua lipo, hivyo huwezi kulibadilisha. Kama utalibadilisha, unafanya kitu fulani ambacho si sahihi.

Katika Zaburi 100:4, tunacho kipengele kingine kinachohusiana kwa hili. ***"Ingieni malango mwake kwa kushukuru; nyuani mwake kwa kusifu: mshukuruni, lihimidini jina lake."*** Na katika Zaburi 135:13: ***"Ee Yahweh jina lako ni la milele; Yahweh, kumbukumbu lako vizazi hata vizazi."*** Hosea 12:5 inasema jambo sawa."Kumbukumbu lako kwa vizazi vyote. Yahweh ndilo kumbukumbu la jina lake." Basi, nini inafanyika wakati mtu anakufuru Jina? Kufuru inamaanisha nini?Ina maana ya *kuongea bila heshima kuhusu jina*.

Adui anafanya hili, kama tulivyoona katika Zaburi 74:10; ***"Ee Yahweh, mtesi atalaumu hata lini?Adui alidharau jina lako hata milele?***[Nini inawafanyikia wale ambao wanakufuru lililo Jina? Vyema, itabidi mwishowe wasimame mbele ya Yahweh.] ***Mbona unaurudisha mkono wako, Naam, mkono wako wa kuume, uutoe kifuani mwako, ukawaangamize kabisa."*** [Yahweh, anawashugulikia watu hawa wanaokufuru lililo Jina.] Mstari wa 18: ***"Ee Yahweh, uyakumbuke hayo, adui amelaumu, na watu wapumbavu wamelidharau jina lako."*** Hivyo watu hawa ni wapumbavu.

Wakati adui anakufuru Jina, nini itamfanyikia yeye? Ufunuo 16:8-9: ***"Na huyo wa nne akakimimina kitasa chake juu ya jua, nalo likapewa kuwaunguza wanadamu kwa moto. Wanadamu wakaunguzwa maunguzo makubwa, nao wakalitukana jina la Yahweh aliye na mamlaka juu ya mapigo hayo; wala hawakutubu wala kumpa utukufu."*** Wakati malaika wa nne anamimina nje bakuli lake juu ya jua, basi kufuru za watu hawa, ambao wanakufuru Jina, wataweza kusoma somo ngumu katika hukumu ya Yahweh.Unaona uhusiano kati ya neno *jua*? ***"Jina lake litadumu kama jua."*** Sasa, kwa sababu wanakufuru Jina la Yahweh, Yahweh anasema, nitaweza kuwaonyeshajua bado liko juu mbinguni, na ilimradi jua na mwezi zinadumu, unatakiwa kuitia Jina la Yahweh katika ibada. Hivyo basi tugeuze jua kiasi. Basi tuangaze jua, na liweze kuchoma watu. Ruhusu wajue kwamba Yahweh ni Aliye Na Nguvu wa Kweli na kwamba unapolitumia vibaya Jina, unapolikataa Jina Lake, unapobadilisha kwa Jina Lake, unakufuru.

Unafanya nini kama unataka kuwa na dharau kwa jina la mtu fulani hapa duniani, katika ulimwengu wetu? Unampa yeye jina la utani, sivyo? Unamwita yeye Ndugu Jake, Bud, au vyovyote.Basi, hivyo ndivyo wamefanya kwa Yahweh. Wamekuwa na dharau kwa Yahweh. Wametumia jina la utani- jina la mbadala- jina ambalo Yahweh hajaidhinisha kwa Jina Lake. Mtu yeyote ambaye anafanya hili ataweza kuhisi kuwaka kwa jua kama Yahweh anawakumbusha wao kwamba jua bado liko nasi kabisa.

Ruhusu turudi nyuma kwa kutumia Jina, Jina ambalo liko katika Neno Lake. Anasema katika Zaburi 75:1: ***"Ee Elohim, twakushukuru; Twakushukuru kwa kuwa Jina lako li karibu; watu huyasimulia matendo yako ya ajabu."*** Hilo ndilo Mzaburi anajaribu kusema hapa, kwamba Jina la Yahweh liko karibu, kwa sababu kazi zake zinalitangaza. Nguvu ya Yahweh inaonyeshwa katika uumbaji Wake.

Ninashangaa kama tunaweza kujiita Waisraeli leo, kwa sababu anasema katika Zaburi 76:1: ***"Katika Yuda Elohim amejulikana, katika Israeli jina lake ni kuu. Kibanda chake pia kiko Salemu, na maskani yake iko Sayuni."*** Jina Lake ni kuu- *gadol*- tena katika Israeli. Ikiwa sisi ni Waisraeli wa siku za kisasa, basi lazima tuwe Waabudu wa Yahweh. Mstari wa 11***: "Wekeni nadhiri, mkaziondoe kwa Yahweh, Elohim wenu. Wote wanaomzunguka wamletee hedaya, yeye astahiliye kuogopwa. Yeye huzikata roho za***

***“Wewe Yahweh, unifundishe njia yako; nitakwenda katika kweli yako: unganisha moyo wangu kulicha jina lako.”***



**Daudi anaitwa mtunga - Zaburi mtamu wa Israeli**

***wakuu; na kuwatisha wafalme wa dunia.”*** Apa na ulipe. Fanya ahadi kwa Yahweh na, kisha itimize. Fanya huko kujitolea kwa Yahweh na utimize. Hilo ndilo kiapo kinamaanisha, “Nimefanya ahadi kwa Yahweh, na nitaweza kutimiza ahadi hiyo.” Zaburi 79:5 ***“Ee Yahweh, hata lini? Utaona hasira milele? Wivu wako utawaka kama moto? Ukali wako uwamwagie mataifa....”*** Basi tuweke neno taifa hapo badala ya *heathens* (kama ilivyo katika toleo la **King James**) kwa neno *goyim* katika Kiebrania ambalo linamaanisha *kundi la kabila*. *Ethnos* katika Kigiriki linamaanisha watu wa *kabila ambalo ni taifa*.

***“Ukali wako uwamwagie mataifa wasiokujua, na falme za hao wasioliitia jina lako.”*** Bila shaka kutakuwa na hukumu. Hili ndilo mzaburi anasisitiza. Hukumu wale ambao hawana hamu kufanya yale Biblia inasema- mataifa, watu ambao wamekataa ujumbe wa kweli wa Biblia- hukumu wao ambao hawajakuwa wakiabudu katika Jina Lako. Kumbuka, Jina la Yahweh ni kuu katika Israeli. Unaona maendeleo ya mawazo hapa? Hii ni kwa nini nimeshawishika kuwa Biblia ni kitabu cha kweli cha Yahweh, kwa sababu mambo kama hayo sio bahati. Roho Mtakatifu wa Yahweh uliongoza kitabu hiki kuwekwa pamoja. Jina la Yahweh ni kubwa katika Israeli. Halitukuzwi, halisifiwi, katika mataifa ya ulimwengu huu, hivyo, wahukumu wao, Mzaburi anasema, mimina ghadhabu yako, hasira yako, hukumu yako juu ya mataifa ya dunia hii, ufalme ambao haulitii Jina Lako kwa sababu sio watu Wako. Wanafanya dhambi.

Katika zaburi 83, unayo Zaburi ya kuvutia sana, na ni unabii kwa wakati wetu katika njia nyingi zaidi ya moja. Ningeweza kusema katika mstari wa 12: ***“Ambao walisema, Na tutamalaki makao ya Elohim. Ee Elohim, uwafanye kama mavumbi ya kisulisuli, mithili ya makapi mbele ya upepo, kama moto uteketezao msitu, kama miali ya moto iiwashayo milima, ndivyo utakavyowafuatia kwa tufani yako, na kuwafadhaisha kwa dhoruba yako. Uwajaze nyuso zao fedheha; iliwakalitafute jina lako, Yahweh.”*** Mataifa ya ulimwengu huu hayajafuata hekalu la Yahweh, nyumba Yake. Hawajafuata Bethel, nyumba ya Elohim. Wamekataa Bethel na Mafundisho safi ya Biblia. Kwa hivyo, mzaburi anasema, ***“Umfanye kama mavumbi ya kisulisuli, mithili ya makapi mbele ya upepo.”*** Umewahi kuona *tumbleweed* katika sehemu ya magharibi mwa Marekani? *Tumbleweed* inaanguka chini ikiendeshwa na upepo, na haiwezi kusimama mpaka ifikie mahali ambapo kizuizi kipo, basi inasimama. Nje katika Magharibi, unaona kando ya barabara kuu za kati malundo makubwa ya *tumbleweed* ambayo yamekuwa yakiendeshwa na upepo dhidi ya ua.Mzaburi anauliza kwa hukumu fulani kali juu ya watu hawa.

***“Uwafanye kama mavumbi ya kisulisuli, mithili ya makapi mbele ya upepo***[kama moto ambao unachoma kuni na hauachi chochote ila majivu.]***kama moto uteketezao msitu.”*** Ninakumbuka nilipokuwa kijana tulikuwa na hali ya hewa iliyokauka sana wakati wa enzi za Dust Bowl. Ninakumbuka babu yangu akinichukua kwenye ghorofa ya pili ya nyumba jioni katika machweo, na tungeweza kunusa kuni zinazochomeka. Tuliangalia kuelekea Blue Mountain, kuelekea Fort Indiantown Gap, na tungeweza kuona kwamba mlima wote- Blue Mountain- ulikuwa unachomeka. Hilo ndilo analozungumza kuhusu. Mwako wa mto mdogo unaweza kuwacha msitu mkubwa- mlima wa misitu.

***“Uwajaze nyuso zao fedheha, wakalitafute jina lako ee Yahweh*** [Lakini inachukua aibu ili mtu aweze kutafuta Jina la Yahweh?] ***Waaibike, wafaidhaike milele; naam, watayaharike na kupotea; na wajue ya kuwa wewe ni Yahweh, ndiwe peke yako Uliye juu, juu ya nchi yote.”*** Yahweh bado ndiye anayeshikilia ulimwengu huu kwenye utupu wa mkono Wake.

Katika Zaburi 86, tena, neno umoja linakuja likipasuka kupitia kwa kifungu hiki- wale ambao wanatumia Jina la Yahweh lazima wawe wameunganishwa. Zaburi

86:11: ***"Wewe Yahweh, unifundishe njia yako; nitakwenda katika kweli yako:unganisha moyo wangu kulicha jina lako."*** Unganisha moyo wangu na wengine wanaoogopa Jina Lako. Kuna umoja tena, katika Jina la Yahweh. ***"Nitakusifu Wewe Yahweh ELohim wangu, kwa moyo wote, nitalitukuza jina lako milele."***

Hatuwezi kuisahau Zaburi 96:4-5, kwa sababu hiki ni kifungu ambacho kinatuelezea kwamba Yahweh, pekee, ni Aliye na Nguvu wa Kweli. Yahweh alifanya kila kitu- ni Muumbaji wa vyote. Kwa hivyo, hakuna Aliye na Nguvu mwingine ila Yeye. Swali mara nyingi inatokea, "Yahweh alitoka wapi?" Kutoka milele, hapo ndipo alitoka! Sisi kama binadamu hatuwezi kuanza kuelewa nini hilo neno linamaanisha. Lazima tusubiri mpaka tuweze pia, kufanywa roho ili tuweze kuielewa. Kama mtu atakuuliza Yahweh alikuja kutoka wapi, basi utamjibu tu: kutoka milele. Zaburi 96:4-5: ***"Kwa kuwa Yahweh ni mkuu, mwenye kusifiwa sana: na wa kuhofiwa kuliko elohim zote. Maana elohim zote za watu ni sanamu, lakini Yahweh ndiye aliyezifanya mbingu."*** Ikiwa tunaamini kwamba Biblia ni ya kweli, basi tutaweza kuondoa majina yote ya upagani kutoka kwa msamiati wetu- kutoka kwa fikra zetu na mawazo.

Zaburi 99:5: ***"Mtukuzeni Yahweh, Elohim wetu, sujuduni penye kiti cha miguu yake; ndiye Mtakatifu. Musa na Haruni miongoni mwa makuhani wake, na Samweli miongoni mwao waliitiao jina lake…."*** Hapa ninataka kutukumbusha, kuabudu penye kiti cha miguu Yake, kama walivyofanya hawa wazee wa kale na manabii. Hili ndilo Mzaburi anajaribu kufikisha. Muinue Yahweh, Mwinue Yeye juu, na kuabudu kwa kiti cha miguu Yake. Usijaribu kumtelemsha yeye chini kwa kiwango chako. Yeye ni mtakatifu- mtakatifu zaidi ya ulivyo, au mimi nilivyo. Kuwa kama Musa na Haruni, ambao walikuwa makuhani wa Yahweh, na kama Samweli mwadilifu miongoni mwao wanaoliitia Jina Lake. Wao ni mifano yetu. Muinue Yahweh juu, na kuinua Yeye! ***"Walipomwita Yahweh aliwaitikia; Katika nguzo ya wingu alikuwa akisema nao. Walishika shuhuda zake na amri aliyowapa. Ee Yahweh, Elohim wetu, ndiwe uliyewajibu; ulikuwa kwao El mwenye kusamehe, ingawa uliwapatiliza matendo yao. Mtukuzeni Yahweh, Elohim wetu; sujuduni mkiukabili mlima mtakatifu; maana Yahweh, Elohim wetu, ndiye mtakatifu."*** (Zaburi 99:6b-9).

Katika Zaburi 111 inapatikana moja ya sababu kwa nini nilichukua cheo cha Mzee badala ya *reverend*( wa kuogopwa). Sikutaka watu wawe wakinirejelea kama wa kuogopwa. Wakati wowote mtu fulani alifanya hili, ninajaribu niwezavyo kumwarifu mara moja kwamba Zaburi 111:9 inasoma ***"Jina lake ni takatifu na la kuogopwa."*** Sio langu. Kunao uhusiano tofauti hapa kati ya mfano wa maombi ya Mwokozi katika Mathayo 6 na Zaburi hii. ***"Maagizo yake yote ni amini. Yamethibitika milele na milele, yamefanywa katika kweli na adili. Amewapelekea watu wake ukombozi, ameamuru agano lake liwe la milele, Jina lake ni takatifu na la kuogopwa."*** Sasa jina takatifu katika Kiebrania ni *qadosh*, na linamaanisha *takatifu, kutengwa na kuogopwa*. Neno lililotafsiriwa *hasira* katika **King James** kweli linamaanisha *kuwa wakuogopwa* na kwa sababu hiyo linapaswa kuwa kuogopa. Nadhani hii ni sababu kwa nini baadhi ya watumishi hawa wanajiita wenyewe wa kuogopwa(*reverend*), ili kwamba watu watawaogopa wao. Nambari 3372 ni *yare'*, na linamaanisha *hofu* (kuogopewa). Tunaweza kuitafsiri kama, takatifu na kuogopewa ni JinaLake. Mstari wa 10 unasema kwamba kumcha Yahweh ni mwanzo wa Hekima. Ni wapi hekima inaanza? Haianzi kwa Jina la Yahweh? Tukipiga magoti yetu mbele ya Yahweh na kusihi kwamba tunaweza kusaidia kuweka Jina Lake takatifu na la kutakaswa na kutengwa. Yahshua katika mfano wake wa maombi, pengine alichukua kifungu hiki kama msingi wa maombi hayo, aliposema, ***"Jina lako litukuzwe."***

Zaburi 113:1: ***"HaleluYah! Enyi watumishi wa Yahweh, sifuni, lisifuni jina la Yahweh. Jina la Yahweh lihimidiwe, tangu leo na hata milele. Toka maawio ya jua hata machweo yake jina la Yahweh ni la kusifiwa."*** Ni wapi Yahweh ataabudiwa? Kote katika sayari hii, kutoka macheo ya jua katika mashariki hadi machweo ya jua katika magharibi, Jina la Yahweh ni la kusifiwa kote katika sayari hii. Kwa hivyo, ni kwa watu wote.

Hapa ni kitu fulani ambacho sio watu wengi hupenda kusikia, lakini, bado, Zaburi 118 inauliza kwamba kiweze kutimizwa. Zaburi 118:8: ***"Ni heri kumkimbilia Yahweh kuliko kuwatumainia wanadamu. Ni heri kumkimbilia Yahweh kuliko kuwatumainia wakuu. Mataifa yote walinizunguka; kwa jina la Yahweh naliwakatilia mbali, walinizunguka, naam, walinizunguka*** [na haikuwa kwa kusudi yoyote nzuri, ilikuwa kwa uharibifu]: ***Kwa jina la Yahweh nitawakatilia mbali. Walinizunguka kama nyuki, walizimika kama moto wa***

***miibani; kwa jina la Yahweh niliwakatilia mbali. Ulinisukuma sana ili nianguke; lakini Yahweh akanisaidia. Yah ni nguvu zangu na wimbo wangu; naye amekuwa wokovu wangu***."

Watakatifu wa Yahweh wanatakiwa kuwa na sehemu katika uharibifu wa mataifa. Zaburi 149:6: ***"Sifa kuu za El na ziwe vinywani mwao, na upanga mkali kuwili mkononi mwao. Ili kufanya kisasi juu ya mataifa, na adhabu juu ya kabila za watu. Wawafunge wafalme wao kwa minyororo, na wakuu wao kwa pingu za chuma. Kuwafanyia hukumu iliyoandikwa; hiyo ndiyo heshima ya watauwa wake wote. HalleluYah."*** Ndio, upanga wenye makali kuwili unatakiwa kuwa mikononi mwetu kila wakati. Upanga wenye makali kuwili haimaanishi kihalisi upanga- kitu cha chuma kilichotiwa makali- ambacho tunaenda kutumia juu ya watu, lakini ni Neno la Yahweh. Unaweza kweli kusimamisha mtu kama Yahweh yu pamoja hapo nawe, kupitia nguvu ya Jina Lake, kwa kuyanukuu Maandiko machache. Inasema katika Kumbukumbu la Torati 28:10, kwamba wataona kwamba unaitwa kwa Jina la Yahweh na watakuogopa wewe. Hivyo wakati unaweza kutumia upanga wenye makali kuwili huo ambao Yahweh ametoa kwako- Neno la Yahweh- unaweza simamisha watu haraka sanasana.

Ninakumbuka moja ya Zaburi yangu ninayoipenda wakati nilienda shuleni- tungeulizwa mara kwa mara kusoma Zaburi katika ibada ya kufungua ya asubuhi. Baadhi ya nilizozipenda zilikuwa Zaburi 24, 124, 100, na 110. Hizi zilikuwa Zaburi ambazo nilihifadhi kutoka ujana wangu, pamoja na Zaburi 1, ambayo kila wakati zilikuwa Zaburi zangu nilizozipenda. Katika *Psalms of Degrees*, Zaburi ambayo iliandikwa na Daudi, ***"Msaada wetu u katika jina la Yahweh, aliyezifanya mbingu na nchi."*** (Zaburi 124:8). Ikiwa Yahweh alifanya mbingu na nchi, basi anayo nguvu ya kutosha kutuhifadhi na kutulinda.


Hatimaye, Zaburi 148. Ningeweza kuipanga hii pamoja na Zaburi za mapema- Zaburi 8- lakini sikutaka kufanya hilo, kwa sababu katika mwishoni mwa Zaburi, unayo taarifa ambayo inajumlisha, pamoja na Zaburi 8 yale tunafikiria kuhusu Jina la Yahweh. Basi na wasifu Jina la Yahweh. Zaburi 148:13: ***"Maana jina lake peke yake limetukuka; adhama yake i juu ya nchi na mbingu. Naye amewainulia watu wake pembe, sifa za watauwa wake wote; wana wa Israeli, watu walio karibu naye."*** Jina lake, pekee ni bora sana. Yeye ndiye pekee aliye na Jina bora duniani humu.

Hivyo msomaji mpendwa, basi tuzingatie Zaburi. Ninatumai kwamba mara kwa mara utazisoma Zaburi na kwamba unazisoma katika tafsiri ambayo ninaamini kuwa tafsiri bora Zaidi iliyopo- **The Sacred Scripture,** *Bethel Edition*. Wakati mwingi hatuoni ukweli mkuu uliopo katika Maandiko. Yahweh ni mchungaji wangu, kwa mfano. Yahweh ni ngao yetu, na Jina lake ni bora sana. Mpango mzima wa wokovu umejumuishwa katika Zaburi. Ni kitabu kikubwa sana, kilichoandikwa na wanaume ambao walikuwa karibu na Yahweh- watu ambao walikuwa na vita vya mara kwa mara kusimama kwa Imani yao, kama alivyofanya Daudi.

Ninatumai kwamba somo hili litakuwa la msaada katika kukuimarisha kiroho- kwamba tutaweza kuona kwamba Jina la Yahweh ni muhimu sana duniani humu. Tunayo jukumu kwa Yahweh kuweka Jina lake safi- kwa kuliinua, kulisifu, kulitukuza, na kulikuza. Na Yahweh atubariki sote kama tunafanya hili, kwa sababu tunaitwa sote kwa Jina Lake. SNB

*"Msaada wetu u katika jina la Yahweh, aliyezifanya mbingu na nchi."*

ZABURI 124:8



***Ikiwa Yahweh alifanya mbingu na nchi, basi anayo nguvu ya kutosha kutuhifadhi na kutulinda.***



# Viumbe vya Yahweh Vilivyoumbwa

SEHEMU 6

**na Mzee Jacob O. Meyer**

Unaposikiliza kwa programu ya Jina Takatifu na kusikia mwandishi akileta ujumbe kutoka kwa Maandiko Matakatifu, utaweza kusikia mambo ambayo huwezi kuyasikia kutoka kwa mwalimu wa wastani katika Ukr-sto. Tunaamini katika kuchukua mtazamo wa kihafidhina kwa kusoma Biblia na kuitafiti, sio kuweka huria yale Biblia inafunza kwa njia yoyote. Tunaamini Maandiko Matakatifu kumaanisha nini yasema; kwa hivyo, lazima tukubali maana iliyo rahisi zaidi, ya msingi zaidi, kutoka kwa maneno yote. Kwa sababu Biblia lazima itafsiriwe na Biblia pekee, lazima tuoanishe Biblia kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Hatuelezei mbali maandishi yoyote yaliyoonyeshwa wazi. Tunayasoma Maandiko katika njia hii, kwamba sababu Biblia inakusudiwa kujumuisha kitengo kimoja kamili. Yohana 10:35 inasema, ***"(na maandiko hayawezi kutanguka)."*** Mwanafunzi wa dhati hawezi kutenganisha biblia kwa Maagano, katika kitabu, kwa mlango, mstari, au neno- kwa sababu Biblia nzima inajumuisha kitengo kimoja kamili, kama tu Mwenye-nguvu Yahweh alinuia iweze kuwa.

Kwa mfano, tunapojadili siku ya sabato leo, Ukr-sto unadai kwamba siku ya kila wiki ya kupumzika ilibadilishwa kutoka siku ya saba ya wiki hadi Jumapili. Kunazo sababu nyingi tofauti ambazo wahubiri mbalimbali na madhehebu wanatoa kwa kuweka kando siku ya saba na kuinua Jumapili kwa nafasi ya Sabato ya kila wiki. Walakini, ni wapi ibada ya jumapili ilianzia? Wapagani wametoa siku hii kwa ibada ya jua kwa milenia mingi. Jina (Sunday) Jumapili halipatikani popote katika Biblia. Siku ya saba ya wiki huanza Ijumaa jioni katika machweo na kuenea hadi Jumamosi jioni katika machweo. Maandiko Matakatifu kwa wazi yanatuarifu kwamba kipindi hiki cha masaa 24 lazima kitunzwe kama takatifu.

Ningependa kusisitiza kwamba katika lugha ya Kihispania, neno la siku ya saba ya wiki ni Sabado. Unatambua kwamba neno *sabato*, linaonyeshwa katika matamshi ya Kihispania? Ni siku ambayo Mwenye-nguvu Yahweh alituambia katika ambayo alipumzika na kuburudika- siku ya saba ambayo aliitakasa.

Ruhusu nikuonyeshe wewe maelezo ya kina sana ya Sabato. Maandishi haya yanapatikana katika Kutoka 31:12-17. ***"Yahweh akasema na Musa, na kumwambia, Kisha, nena wewe na wana wa Israeli, na kuwaambia, hakika mtazishika sabato zangu."*** Sasa, vipi tunaweza kuweka kando amri hii wakati Yahweh, Muumbaji, Baba Sheria na manabii, lakini nilikuja kutimiza Sheria," kuitunza sheria na manabii na kuishi kwa kila Neno. Tena, katika Kutoka 31:12, tunapata, ***"Hakika mtazishika sabato zangu."*** Yahweh anatuagiza kwa wazi kutunza amri ya nne. Waabudu wa Kweli wana wajibu, hadi kwa siku hii hasa kutunza amri ya nne, kuadhimisha siku katika ambayo Mwenye-nguvu Yahweh alipumzika na akaburudika kutoka kwa siku Zake sita za uumbaji. Siku ya Sabato kamwe haijawahi kupotea chini kote katika historia. Kila wakati imekuwa siku ya saba ya kila wiki. Wakristo wanatangaza kwamba wanaitunza siku ya kwanza ya kila wiki katika heshima kwa ufufuo wa Messiah; kwa sababu hiyo ya Biblia kuwaambia wao kuibadilisha, waliifanya tu! Katika ibada ya kale, Jumapili ilikuwa siku ya Bw-na, au Baali, siku katika ambayo Bw-na aliabudiwa, siku ya Bw-na. Mabaali walikuwa Mabw-na wa eneo, kama matokeo yake basi, Ukatoloki ulichukua siku hiyo, na wakaibadilisha siku ya kupumzika.

Hapa, katika Kutoka 31:13, Maandishi yanaendelea. ***"Kwa kuwa ni ishara kati ya mimi na ninyi katika vizazi vyenu vyote, ili mpate kujua ya kuwa mimi ndimi Yahweh niwatakasaye ninyi."*** Mwenye-nguvu Yahweh alituamuru sisi kutunza Sabato. Pia alituarifu kwamba lazima tuitunze kote kupitia vizazi vyote ***"Basi mtaishika hiyo Sabato;*** ***kwa kuwa ni takatifu kwenu; kila mtu atakayeitia unajisi hakika yake atauawa; kwa kuwa kila mtu afanyaye kazi katika siku hiyo, nafsi hiyo itakatiliwa mbali na watu wake."*** Kauli hii ni wazi kabisa, rahisi, na dhahiri, sivyo? Mwenye-nguvu Yahweh aliwaambia watu Wake waitunze Sabato (siku ya saba ya wiki). Aliwaambia watu Wake kwamba hakuna kazi ambayo lazima ifanywe siku hiyo. ***"Kazi ifanywe siku sita; lakini siku ya saba*** [siku ya saba ya wiki ni siku takatifu ya Yahweh, ambayo ametakasa kwa ibada Yake mwenyewe na kamwe hakubadilisha***]*** ***ni Sabato ya kustarehe kabisa,***

***Tunaamini katika kuchukua mtazamo wa kihafidhina kwa kusoma Biblia na kutafiti, sio kuweka huria yale Biblia inafunza katika njia yoyote. Tunaamini Maandiko Matakatifu kumaanisha nini yasema; kwa hivyo, lazima tukubali maana iliyo rahisi zaidi, ya msingi zaidi, kutoka kwa Maneno yote.***

Mwenye-nguvu wa Mbinguni anasema LAZIMA MTUNZE SABATO ZANGU? Tutabadilisha siku kwa kurekebisha neno sabato kwa neno Mkristo, kama baadhi ya madhehebu yanavyofanya? Au tutasema tu kwamba wakati aliye Mesiah alikufa, aliweka kando Sheria ya kimaandiko kuibadilisha kwa ambayo si ya kimaandiko? Katika Mathayo 5:17 aliye Messiah anatangaza kwamba hakuja kutangua Sheria. Kama utaangalia neno la Kigiriki la kutangua, utaweza kupata ni *luo* ambalo linaonekana kama neno la mzizi, na linamaanisha kubatilisha. Yahshua aliye Messiah alisema "Sikuja **kutangua** (au **kubatilisha**), wanatambua siku ya saba ya kila wiki na pia siku ya kwanza. Kwa hivyo, Ukr-sto umefanya maamuzi kuhamisha utakatifu kutoka kwa siku ya saba na kutunza Jumapili. Walakini, HAKUNA KABISA AMRI POPOTE KATIKA BIBLIA kubadilisha siku ya kupumzika na kuabudu kutoka Sabato hadi Jumapili.

Wakati tunaanza kuelewa ukweli huu, basi lazima tujiulize sisi wenyewe lililo swali, "Ni nani alibadilisha siku ya kupumzika na kwa mamlaka gani walifanya hili?" Ukatoliki unajiita wenyewe kasisi wa Messiah duniani leo, na, kwa mamlaka haya, wamebadilisha iliyo siku. Hakuna marejeleo

***takatifu kwa Yahweh; kila mtu akatakayefanya kazi yo yote katika siku ya Sabato hakika yake atauawa. Kwa ajili ya hayo wana wa Israeli wataishika Sabato, kuiangalia sana hiyo sabato katika vizazi vyao vyote, ni agano la milele. Ni ishara kati ya mimi na wana wa Israeli milele; kwani kwa siku sita Yahweh alifanya mbingu na nchi, akastarehe kwa siku ya saba na kupumzika."***Mwenye-nguvu Yahweh anakusudia kwamba tutakuwa na ishara inayounganisha Waabudu wa Kweli Kwake; kwa hivyo, ishara hiyo ni Sabato. Dini ya kidunia haifunzi Ukweli huu, na viongozi wake wanawapoteza watu kwa mafundisho ya uwongo (angalia Hosea 4:6). Hiyo ndiyo sababu nilitoka nje ya Ukr-sto, na, zaidi ya miaka 40 iliyopita, kujiunga katika njia ya kurejesha Ukweli wa kibiblia na kutii Baba wetu Mbinguni kwa moyo wangu wote.

Nimekuwa nikizungumzia juu ya mada ya madarasa manne ya viumbe vilivyoumbwa ambavyo Mwenye-nguvu Yahweh aliumba kuwa watumishi Wake. Darasa la kwanza ambalo tulijadili, bila shaka, lilikuwa *makerubi*. Kisha wakaja *maserafi* na *malachim*, ambao ni *malaika*, au *angelos*, kama Kigiriki kingeweza kuitoa.

Malaika hao (Kiebrania, *malachim*) ni wajumbe wa Yahweh. Aliwaumba wao kumtumikia Yeye duniani humu, kuwaangalia binadamu, na kuripoti tena Kwake katika Mbingu. Kila kitu mnachokifanya marafiki, kinaripotiwa kwa Mwenye-nguvu Yahweh Mbinguni, na malaika wake wanatuangalia. Kama kunayo shida maalum, anaweza kutuma kundi la malaika kuchunguza kwa niamba yake, kama alivyofanya katika Mwanzo 18 na 19, wakati alituma malaika watatu kuchunguza ikiwa dhambi za Sodoma na Gomora zilikuwa zinaendelea. Alisema kwamba kilio cha Sodoma na Gomora kilikuwa kimefika mbele Yake. Kwa hivyo, utaweza kuamini kwamba malaika waliripoti, na basi, Mwenye-nguvu Yahweh alitaka kujua habari zaidi, hivyo akamtuma Yahweh wa pili-Mwana Wake, malaika huyu maalum, ambaye baadhi ya wakati anaitwa Elohim na wakati mwingine anaitwa Yahweh. Malaika huyu na wengine wawili kwanza walimtembelea Ibrahimu. Kisha malaika wawili walitelemka Sodoma ambapo walichunguza mwenendo wa Sodoma, kuamua kuzorota kwa kutisha vipi kulikuwa kumekamata udhibiti wa Sodoma katika wakati huo na kisha kuripoti tena kwa Yahweh.

Ningependa kuangalia kwa kina zaidi kwa malaika huyu maalum anayerejelewa katika Ufunuo 10. Wakati mwingi madhehebu ya kidini hawawaruhusu watumishi wao hata kutumia kitabu cha Ufunuo. Wanashindana kwamba kitabu ni chenye utata sana. Pengine mlango wa 1 na 22 unaweza kukubaliwa, lakini mingine yote ya Ufunuo ni yenye utata tu. Hawawezi kuielewa au kuielezea, wanadai. Katika Assemblies of Yahweh, hili sivyo ilivyo. Mwenye-nguvu Yahweh ametupa Roho Wake Mtakatifu, na amefanya wazi kusudi kwa ambalo amekusanya kitabu cha Ufunuo. Anataka sisi kukisoma, kutafakari, na kuelewa kitabu hiki cha kinabii, ili kwamba tunaweza kuchukua onyo na kuwa tayari kukabiliana na siku za mwisho. Kitabu cha Ufunuo ni antholojia kweli ya unabii wa nyakati za mwisho ambao Mwenye-nguvu Yahweh ametawanya kote katika Biblia iliyobaki. Unabii huo basi ulikusanywa na kuwekwa kwenye mpangilio sahihi katika kitabu cha Ufunuo. Hili limeweza kufanyika chini ya mwanga na msukumo wa Mwenye-nguvu Yahweh, Baba wetu katika Mbinguni, kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu.

Geukia kwa Ufunuo 10. ***"Kisha nikaona malaika mwingine mwenye nguvu akishuka kutoka mbinguni, amevikwa wingu; na upinde wa mvua juu ya kichwa chake, na uso wake ulikuwa kama jua, na miguu yake kama nguzo za moto."*** Sasa hili linazungumzia kuhusu nini? Kwanza kabisa, tunabaini kwamba anateremka kutoka mbinguni. Tunaporudi nyuma kwa Matendo ya Mitume 1:9-11, tunasoma, ***"Akiisha kusema hayo, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao. Walipokuwa wakikaza macho mbinguni, yeye alipokuwa akienda zake, tazama, watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe, wakasema, Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yahshua aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni."*** Katika Ufunuo 1:7, tunapata: ***"Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma; na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake. Naam, Amen."***

Basi tuangalie karibu zaidi kwa jinsi anaelezewa katika Ufunuo 1:13. ***"Na katikati ya vile vinara nikaona mtu mfano wa mwanadamu, amevaa vazi lililofika miguuni, na kufungwa mshipi wa dhahabu matitini. Kichwa chake na nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu nyeupe, kama theluji; na macho yake kama mwali wa moto. Na miguu yake kama shaba iliyosuguliwa sana, kana kwamba imesafishwa katika tanuri; na***

***sauti yake kama sauti ya maji mengi"*** Utagundua nini Ufunuo 10 inaelezea kwa kuzingatia tu Maandishi haya kadhaa. Inaelezea Ujio wa mara ya Pili wa Yahshua aliye Messiah; walakini tunapaswa kuuliza kwa nini anaitwa malaika? Mtu wa wastani hatambui kuwa Yahweh, Baba wetu katika Mbinguni alikuwa na Msemaji, msemaji maalum, ambaye alikuwa ameumba kwa kusudi hili. Yeye ni malaika(mjumbe) wa msingi anayeongoza. Yeye ndiye anayeamuru jeshi lote la malaika katika Maandiko Matakatifu. Kama matokeo yake, Messiah ndiye anaitwa Mica-el au Mikaeli.

Basi tugeukie kwa Danieli 12:1. ***"Wakati huo Mikaeli atasimama, jemedari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo; na wakati huo watu wako wataokolewa, kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile."*** Jina *Mikaeli* linalo maana ya kuvutia sana katika lugha ya Kiebrania. Jina Mikaeli linavyo vipengele vitatu. Kipengele cha kwanza ni *Mi*, ambacho ni chembe cha kuhoji ambacho kinahudumu kama alama ya kuuliza, *nani au nini* (katika tukio hili *nani*). Kisha kuna *ch* au *k* ambayo ni *kaph* katika Kiebrania na ni kihusishi. Kinamaanisha *kama*. Kipengele cha mwisho ni *el*. Neno *el* ni ufupisho wa neno Elohim, hivyo jina linauliza swali, "*Ni nani kama Elohim?"* Jibu ni mwana Wake wa pekee, kwa sababu ya nini tunasoma katika Ufunuo 3:14. Yeye ni mwanzo wa uumbaji wa Yahweh. Hilo linamaanisha Yeye ni Kiumbe aliyekaribia zaidi kwa Muumba, na amejaliwa na zawadi hizi kuu na nguvu kama Mwana mzaliwa wa pekee wa Yahweh Elohim.


Je, Ufunuo sio kitabu kikubwa tu? Nafurahia kila wakati tunaona mambo kama haya na kila wakati ninayahakiki na kuhubiri mahubiri juu ya mada hizi. Siwezi jizuia ila kuonyesha mambo haya kwa ulimwengu, kwa sababu ninayapenda, na ninafurahia kwa kitabu hiki, kwa sababu kinajielezea chenyewe.

Kwa sababu hiyo, katika Ufunuo 10:2, tunasoma, ***"Na katika mkono wake alikuwa na kitabu kidogo kimefunguliwa. Akaweka mguu wake wa kuume juu ya bahari, nao wa kushoto juu ya nchi…."*** Hili linamaanisha aliweka mguu wake wa kuume juu ya bahari na mwingine juu ya nchi, na akaweka dunia nzima kwenye utiifu wa utawala na nguvu Yake. Hilo linamaanisha kwamba alikuwa ameshinda dunia nzima, hivyo kwamba dunia yote iko chini ya mamlaka yake. ***"Naye akalia kwa sauti kubwa kuu, kama simba angurumavyo.Na alipolia, zile ngurumo saba zikatoa sauti zao."***


***"Hata ngurumo saba zilipotoa sauti zao, nilikuwa tayari kuandika: nami nilisikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Yatie muhuri maneno hayo yaliyonenwa na hizo ngurumo saba, usiyaandike."***

Hatujui nini ngurumo saba zilisema, ingawa zaburi ya "ngurumo saba" inaonekana katika Zaburi 29. Tunaweza kuhesabu ngurumo hizi saba na kutazama matokeo ya nini inafanyika wakati Yahweh anaongea. Huyu ni Yahweh anaongea na sauti Yake ni kama sauti ya ngurumo. Anapozungumza, mambo yanafanyika!

Kwa sababu hiyo, malaika huyu anacho kitabu, na hicho kwa kweli ni kitabu kidogo kulinganisha na baadhi ya vitabu tunavyotumia katika Obadiah School of the Bible. Ni cha kueleweka sana, kwa sababu ni wazi hivyo na kwa kifupi. Unaweza kuelewa yale kinasema, kutuwezesha sisi sote kujifunza na kuoanisha ujumbe wake.




Tunasoma katika mstari wa 5, ***"Na yule malaika niliyemwona, akisimama juu ya bahari na juu ya nchi, akainua mkono wake wa kuume kuelekea mbinguni, akaapa kwa yeye aliye hai hata milele na milele, yeye aliyeziumba mbingu na vitu vilivyomo, na nchi na vitu vilivyomo, na bahari na vitu vilivyomo, ya kwamba hapatakuwa na wakati baada ya haya:*** [Yahweh sasa ataweza kuchukua nguvu yake ya kutawala] ***lakini katika siku za sauti ya malaika wa saba atakapokuwa tayari kupiga baraghumu, hapo ndipo siri ya Elohim itakapotimizwa, kama alivyowahubiri watumishi wake hao manabii. Na sauti ile niliyoisikia kutoka mbinguni ilinena nami tena, ikisema,***



*Mpeni Yahweh, enyi wana wa Yahweh,*
*Mpeni Yahweh utukufu na nguvu;*
*Mpeni Yahweh utukufu wa jina lake;*
*mwabuduni Yahweh kwa uzuri wa patakatifu pake.*
*SAUTI YA YAHWEH I juu ya maji;*
*Elohim wa utukufu alipiga radi; Yahweh yu juu ya maji mengi.*
*SAUTI YA YAHWEH in a nguvu;*
*SAUTI YA YAHWEH ina adhama;*
*SAUTI YA YAHWEH yaivunja mierezi, naam, Yahweh Ai vunja-vunja mierezi ya Lebanoni.*
*Airusha-rusha kama ndama.*
*Lebanoni na Sirioni kama mwana-nyati*
*SAUTI YA YAHWEH yaipasua miali ya moto.*
*SAUTI YA YAHWEH yalitetemesha jangwa,*
*Yahweh alitetemesha jangwa la Kadeshi.*
*SAUTI YA YAHWEH yawazalisha ayala, nakuifichua misitu na ndani ya hekalu lake wanasema wote, utukufu.*
*Yahweh aliketi juu ya gharika; naam, Yahweh hali ya mfalme milele.*
*Yahweh atawapa watu wake nguvu;*
*Yahweh atawabariki watu wake kwa amani.*

***enenda, ukakitwae kile kitabu kilichofunguliwa katika mkono wa Yule malaika, aliyesimama juu ya bahari na juu ya nchi.*** " Kitabu hakijafungwa tena. Yahshua aliye Messiah mwanakondoo wa Yahweh, ameshinda kufungua kitabu, tunaambiwa katika mlango wa tano wa kitabu cha Ufunuo.

Yohana aliambiwa achukue kitabu kidogo na akile. Katika Ezekieli 3:1-3 linaonekana tukio sawa ambapo nabii Ezekieli anaambiwa ***"kitwae kitabu, ukile."*** Ni wazi, mtu hachukui chumvi, pilipili, na achali rojo na kuuma vipande vipande kihalisi kutoka kwa kitabu hiki. Walakini, ni sawia kwa chapisho la **Reader's Digest**. Chapisho hilo linatoa mali ya kula baadhi ya kazi maarufu zaidi ambazo zimeweza kuandikwa kwa ajili ya wakati wetu. Unaweza kusoma kitabu na kisha kiishara kukisaga. Hilo ndilo maandishi yananuia kwetu kuelewa. Tunasoma kitabu, kukisaga, kukifanya sehemu yetu wenyewe, kuiweka kwenye akili zetu, kuishi kwake, na kuiweka vitendoni. Hili ndilo ambalo inasema

***"Nikamwendea malaika Yule nikamwambia kwamba anipe kile kitabu kidogo. Akaniambia, kitwae, ukile, nacho kitakutia uchungu tumboni mwako, bali katika kinywa chako kitakuwa kitamu kama asali. Nikakitwaa kile kitabu kidogo katika mkono wa malaika Yule, nikakila, nacho kikawa kitamu kama asali kinywani mwangu, na nilipokwisha kukila tumbo langu likatiwa uchungu. Wakaniambia, imekupasa kutoa unabii tena juu ya watu na taifa na lugha na wafalme wengi."*** Anafanya hilo sasa hivi kama nasoma kitabu hiki. Anatabiri kupitia Neno Lake lililorekodiwa.

Ni kitabu kitukufu kama nini cha Ufunuo! Kwa sababu Yahweh anatupenda sisi na anataka sisi kuwa watoto Wake, ametoa Mwana Wake, ambaye alikuwa Malaika mkuu wakati mmoja, kuwa Mwokozi wetu. Tutarudisha upendo wetu katika utiifu Kwake? Yahshua aliishi na kufunza kwamba hii ndiyo njia ya wokovu, na alituonyesha sisi, kupitia kwa Mfano Wake, jinsi tunaweza kuwa watumishi (Obadiahs) wa Baba wetu na Muumba, Yahweh. Kuwa mtumishi wa Yahweh limekuwa lengo langu kwa zaidi ya miaka 40; kwa hivyo, ninatumai kwamba utaungana nasi kama unatafuta kumfuta Mwanakondoo wa Yahweh kila siku. Andika kwa Assemblies of Yahweh, PO Box C, Bethel, PA 19507. Omba maandishi yetu ya bure. Amua kwako mwenyewe kwamba Assemblies of Yahweh sio dhehebu.

PART 6



# Messiah katika Agano la Kale

**na Mzee Jacob O. Meyer**

Kila mtu anaonekana kuwa na wasiwasi kuangalia kwenye siku zijazo. Hilo ndilo pengine ni kwa nini watu wengi leo wanatumia pesa katika bodi za Ouija, au kuenda kwa wapiga ramli. Watu wengi wanatazama utabiri wa kila siku wa unajimu. Wanatafuta kuangalia katika siku zijazo. Watu kama hao ambao wanatumia njia kama hizo za kidunia kutazama kwenye siku zijazo pengine wangekejeli unabii wa Biblia, ambao hata hivyo, ungekuwa sahihi zaidi kwao kuamini.

Niko hapa leo kutangaza kwamba unaweza kutegemea zaidi juu ya unabii wa Biblia kuliko unavyoweza juu ya bodi za Ouija, wapiga ramli, au utabiri wa Unajimu ambao unaonekana kila siku katika gazeti! Biblia yako ni kitabu cha kuaminika. Kiliwekwa

kwa uwepo na Mwenye-nguvu ili kwamba tunaweza kuangalia kwenye siku zijazo na kupanga maisha yetu kulingana kwa yale kinayoamuru. Unabii wa Biblia unaifanya Biblia kuwa ya kufaa leo kwa kila mmoja wa wasomaji.

Mwenye-nguvu Yahweh, alipomweka binadamu humu, hakumweka hapa bila ya kumpa aina fulani ya maagizo pia. Yahweh, kwa kujiondoa Mwenyewe kutoka kwa uumbaji Wake, angeweza kuleta basi hali sawa kwa kumlea mtoto katika utupu bila ya muungano na mtu mwingine na bila ya mtoto kuwa na uwezo wa kuwa na uzoefu wowote wa maisha. Mwenye-nguvu Yahweh hakufanya hilo kabisa. Hakuwaacha, au kujiondoa Mwenyewe kabisa kutoka kwa uumbaji Wake kabisa. Aliwapa wao maagizo kwa maisha

Maandiko Matakatifu yanatuarifu sisi katika Mwanzo 2:16 kwamba Mwenye-nguvu Yahweh "**Alimwamuru mtu**," na amri hizo bado zinaweza kupatikana zimeratibiwa kwetu katika Biblia. Zimeweza kurekodiwa katika Torati (Sheria) za Maandiko. Yahweh aliamuru mtu Yule, na mtu alihitajika kutii. Walakini, mwanamume na mwanamke hawakutii, lakini walikataa serikali ya Yahweh- maagizo aliyowapa wao na mamlaka yake juu yao. Kwa hivyo, walikubali utawala na kutawala kwa Shetani, kupitia ambako walipoteza urithi wao waliopewa na Yahweh, ambao ulikuwa bustani la Edeni.

Leo tunatafuta kurejesha Ukweli wa Aliye Juu duniani humu. Tunaangalia mbele kwa ufalme wa Yahweh kuanzishwa kote duniani humu. Baadhi ya watu tayari wamejitolea kwa hiari wenyewe kwa serikali hiyo. Sisi, washiriki wa Assemblies of Yahweh, tunaishi maisha yetu katika maelewano na Neno la Yahweh, tukitumai kwa kuonekana huko kwenye utukufu kwa Yahshua aliye Messiah kutoka Mbinguni kutawala dunia hii katika haki.

Vipi tunaweza kusema kwamba Mwanamume wa Galilaya, anayeelezewa katika Agano Jipya, kwa kweli alikuwa Messiah wa Israeli na wa ulimwengu? Umeweza kuzingatia swali kama hili? Mwanamume wa Agano Jipya kweli alikuwa Aliye Messiah wa Israeli na ulimwengu?Vipi unaweza kuthibitisha kwa ukamilifu kwamba alikuwa Messiah wetu? Jibu linapatikana katika yanayoitwa Maandiko ya Agano la Kale. Agano la Kale- maandiko ya Kiebrania- kweli yanajumuisha msingi wa Imani yetu, na hapo ndipo unabii wa kimessiah ni wa kupatikana katika mpangilio wake wa asili.

Yahshua aliye Messiah anaonekana katika Maandiko ya Agano Jipya sawasawa kama alivyotabiriwa kufanya katika Agano la Kale. Agano Jipya ni mkusanyiko wa maandishi yaliyokusanywa kuthibitisha kwamba Yahshua kweli alikuwa Messiah. Kama ungetaka kugeuka kwa Yohana mlango wa 21, utapata kwamba Yahshua alikuwa mhusika wa kati wa maandishi ya Yohana. Yohana aliandika Habari Njema yake (na baadaye waraka wake) kuthibitisha pasipo shaka kwamba Yahshua alikuwa Messiah.

Basi tusome Yohana 21:24-25, ***"Huyu ndiye Yule mwanafunzi aliyeyashuhudia haya, na aliyeyaandika haya: nasi twajua ya kuwa ushuhuda wake ni kweli. Kuna mambo mengi aliyoyafanya Yahshua; ambayo yakiandikwa moja moja, nadhani hata ulimwengu usingetosha kwa vile vitabu vitakavyoandikwa."*** Hapa, Yohana aliye Mtume anasema kwamba aliandika kitabu chake cha Habari Njema kuonyeshwa kwamba Yahshua alikuwa Messiah na kushuhudia kwamba Messiah alikuwa amekuja duniani humu. Yohana alitoa ushahidi wake wa kweli kwamba alikuwa amemwona aliye Messiah.

Ruhusu pia tusome Yohana 20:30-31: ***"Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yahshua mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yahshua ndiye Messiah, Mwana wa Yahweh; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake."*** Wasomaji hao ambao wanamilki Biblia nzuri ya kusoma, toleo ambalo linabainisha matukio ambayo Agano Jipya linanukuu kabisa na moja kwa moja kutoka kwa maandishi ya Agano la kale, watajua kwamba Yohana alinukuu mara kwa mara kutoka kwa Maandishi ya Kiebrania- Agano la Kale. Kama utageukia kwa Yohana 19, kwa mfano, utapata hapo kwamba idadi ya nukuu zinaonekana. Wakati Yahshua aliagikwa juu ya mti wa Kalvari, ilikuwa katika utimilifu wa unabii wa Biblia.

Ni wapi tunapata kwamba Yahshua aliye Messiah alikuwa ametimiza unabii wa Biblia? Yahshua alisema kwamba alitabiriwa katika sheria (*Torah*), Manabii (*Nabi'im*), na Zaburi (*Kethubim*). (Biblia nzima ya Kiebrania inajulikana kwa kifupi-TaNaK- kwa sehemu hapo juu.) Kote katika Maandiko ya Agano la Kale, tutapata Yahshua aliye Messiah ametabiriwa.

Umewahi kujionea mambo haya kwako mwenyewe? Umewahi kuona jinsi alivyotabiriwa hasa na jinsi alivyotimiza unabii huu? Ruhusu tuangalie tu kwa moja ya Maandiko. Katika Zakaria 9:9, tunapata utabiri wa jinsi Yahshua angeingia kwenye Mji Mtakatifu. ***"Furahi sana, Ee binti Sayuni;***

***piga kele, Ee binti Yerusalemu: tazama, mfalme wako anakuja kwako; ni mwenye haki, naye ana wokovu; ni mnyenyekevu, amepanda punda, Naam, mwana-punda, mtoto wa punda."*** Yahshua aliye Messiah alitimiza unabii huo kikamilifu.


Lakini ni kwa nini watu walimtambua Yeye kama Messiah aliposafiri juu ya punda kuenda Yerusalemu? Basi tusome hilo katika Luka mlango wa 19, kuanzia kusoma katika mstari wa 29. ***"Ikawa alipokaribia Bethfage na Bethania, kwenye mlima uitwao wa Mizeituni, alituma wawili katika wale wanafunzi, akisema, nendeni mpaka kijiji kile kinachowakabili, na mtakapoingia ndani mtaona mwanapunda amefungwa ambaye hajapandwa na mtu ye yote bado, mfungueni mkamlete hapa. Na kama mtu akiwauliza, Mbona mnamfungua? Semeni hivi, Mwalimu anamhitaji. Na wale waliotumwa wakaenda wakaona kama alivyowaambia. Na walipokuwa wakimfungua mwanapunda, wenyewe waliwaambia, Mbona mnamfungua mwanapunda? Wakasema, Mwalimu ana haja naye. Wakampeleka kwa Yahshua, wakatandika nguo zao juu ya mwanapunda, wakampandisha Yahshua. Na alipokuwa akienda walitandaza nguo zao njiani. Hata alipokuwa amekaribia matelemko ya mlima wa Mizeituni, kundi nzima la wanafunzi wake walianza kufurahia na kumsifu Elohim kwa sauti kuu, kwa ajili ya matendo yote ya uwezo waliyoyaona, wakasema, Ndiye mbarikiwa Mfalme ajaye kwa jina la Yahweh; amani mbinguni, na utukufu huko juu."***

Baadhi ya akaunti zingine zinasema kwamba watu walilia *hoshi'ahnna*, au *Hosanna*, maana yake*, Okoa sasa, ee Yahweh.*

Umeweza kutambua maandishi ya nyongeza kutoka kwa Agano zote ya Kale na Jipya? Hapa, tunao unabii mara mbili wa siku zijazo kama unavyoonekana katika Zakaria 9:9 na utimilifu sahihi unaopatikana katika Luka 19:29-38. Yahshua aliye Messiah kwa usahihi alitimiza unabii. Alikuja amepanda punda ndani ya Yerusalemu katika Kuingia Kwake kwenye Ushindi. Kitukio, siku ambayo Yahshua alikuja akipanda punda kuingia Yerusalemu haikuwa Jumapili ya Mitende. Leo, mak-nisa ya kidunia huadhimisha tukio hili katika Jumapili ya Mitende, lakini kamwe halikufanyika katika Jumapili ya Mitende. Ilifanyika katika siku ya kumi ya Abibu, siku ambayo mwanakondoo alichaguliwa kwa huduma ya Pasaka (Kutoka 12:3), Sabato kabla ya kutundikwa kwake katika Jumatano iliyofuata, Abibu 14.

Ningependa kukuhimiza wewe kuzingatia mafundisho safi ya Biblia. Moja ya mafundisho hayo safi ni kutunza amri za Yahweh. Tunapotunza amri za Yahweh, basi tunatambua kwamba mafundisho yote yanayofunzwa katika Maandiko ni kweli, na kwamba baadhi ya mafundisho ambayo yanatangazwa na madhehebu ya dini za kidunia yako katika makosa. Tunasita kumlaani yeyote, lakini ni ukweli dhahiri kwamba mafundisho yanayofunzwa katika ukr-sto leo hayalingani, au kuhusiana na yale yaliyoandikwa katika Neno la Yahweh. Miongoni ya hayo ni fundisho hili la kutundikwa Ijumaa na ufufuo wa Jumapili, ambalo haliwezi kuungwa mkono kutoka kwa Maandiko Matakatifu.

Sasa, ningependa kukuonyesha ukweli wa kauli hiyo kwa kifupi, na hili linapatikana katika unabii mwingine. Katika Mathayo




12:39-40, Yahshua aliye Messiah anatoa ishara kama uthibitisho wa umessiah Wake kwa wanafunzi Wake na kwa Mafarisayo. Mafarisayo haswa walikuja kwake na kumuuliza ishara. Alisema kwao, ***“Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara, wala hakitapewa ishara, ila ishara ya nabii Yona: kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la samaki mkubwa; hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu na kucha tatu katika moyo wa nchi.”*** Ndio, Yahshua aliye Messiah kweli aliweza kutimiza unabii huo.

Tunapogeuka kwa Yona 1:17, tunatambua kwamba unabii ulitolewa katika wakati Yona alirushwa baharini kutoka kwa merikebu iliyopigwa na dhoruba, na alimezwa na samaki mkubwa. Alikuwa ameagizwa na Mwenyenguvu Yahweh aende Ninawi kuhubiri toba kwa Waashuri, lakini alichukua merikebu iliyoenda katika mwelekeo tofauti kabisa na Ninawi. Mwenye-nguvu Yahweh alileta dhoruba kubwa, na wenzake Yona katika merikebu wakamrusha nje ya merikebu kutuliza nguvu za majini, kwa sababu aliwaambia, “Mimi ndimi mtu aliye na uwajibikaji kwa shida zenu zote katika wakati huu wa sasa.” Yona 1:17 inasoma, ***“Yahweh akaweka tayari samaki mkubwa*** [*dag gadol*- samaki mkubwa sio nyangumi] ***ili ammeze Yona, naye Yona akawa ndani ya tumbo la samaki yule muda wa SIKU TATU, na KUCHA TATU.”***

Rafiki, umewahi kuzingatia unabii huu? Vipi mtu yeyote anaweza kuhesabu siku tatu kamili na kucha tatu kamili kutoka Ijumaa hadi Jumapili? Ni isiyowezekana! Na, bado makanisa ya kidunia leo yanatunza Jumapili ya Mitende, Ijumaa Njema, na Jumapili ya Easter kama maadhimisho takatifu. Biblia kamwe haizitangazi kuwa takatifu, lakini inatufunza maadhimisho ya siku za sikukuu za Walawi 23!

Yahshua ni Messiah wa Israeli kwa sababu alitimiza unabii wa Maandiko ya Agano la Kale. Kama moja ya unabii huu ulikuwa umeshindwa, madai Yake yangeweza kuwa katika shaka. Walakini, Yahshua mwana wa Yusufu wa Nazareti alitimiza unabii huu wote; kwa hivyo, amethibitishwa kuwa Messiah.

Basi na tuthibitishe imani yetu katika Messiah kwa kuamini Neno la Aliye Juu, Baba aliye Mbinguni-Yahweh- na kwa kuishi katika maelewano na njia yake ya maisha. Kwa kusoma Biblia, tutaweza kuingia Ufalme wa milele wakati Yahshua anarudi kuwakusanya wachaguliwa Wake. SNB




***Hapa ni chapisho ndogo la mfukoni utakapopata sababu ni kwa nini Ukristo wa kidunia kwa kweli umemkataa aliye Messiah kwa kukosa kutambua ishara ya pekee aliyotoa-siku tatu na kucha tatu katika kaburi-kuthibitisha yeye ni Mfalme wa Yahweh.***

*Kwa habari zaidi jinsi ya kupata kopi yako ya utafiti huu wa kuelimisha, andika kwa:*

**Assemblies of Yahweh**
**PO Box C, Bethel, PA 19507**
**www.assembliesofyahweh.com**

*Sacred Name Broadcaster*
*Bethel, PA 19507*

PERIODICAL
Reading, PA

# Vyombo vyako Bora vya Kujifunza Biblia




# WMLK Radio

## Assemblies of Yahweh Shortwave

**Now Broadcasting 6 DAYS A WEEK**

**15150 kHz 1200-1700 GMT (8 AM - 1 PM EDT)**
**17525 kHz 1730-2230 GMT (1:30 PM - 6:30 PM EDT)**
**9275 kHz 2300-0400 GMT (7 PM - 12 Midnight EDT)**

**On the air 24/7 at WMLKRadio.com, on TuneIn.com or at station.voscast.com/5cfe89883c143**

(Note: There are times that WMLK is not broadcasting because of maintenance or repairs.)